هذا هو الإسلام - سواحيلي

# Huu ndio Uislamu




جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ - فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# HUU NDIO UISLAM

## هذا هو الإسلام - سواحيلي


KIMETAFSIRIWA NA KUHAKIKIWA NA:

1- ALLY NASSOR ALLY

2- ABDALLAH CHUMBE

3- ABUBAKAR KASSIMU ABUBAKAR



جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي

هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# هذا هو الإسلام - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**

**ⓗ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ**

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
هذا هو الإسلام / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ

٩٢ ص ؛ ..سم

ردمك: ٦-١٥-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الاسلام ٢- التوحيد أ.العنوان

ديوي ٢١٠ ١٤٤٤/٥٨٢٨

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٢٨**
**ردمك: ٦-١٥-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Mtu anapoifikiri ardhi na akauona ulimwengu huu ulio mkubwa na mzuri, mbingu na nyota zake zilizo nyingi, zote zikienda kwa mpango madhubuti, na ardhi na milima yake na mabonde na mito, miti, mimea, hewa, maji, nchi kavu na bahari, mchana, usiku, yote hayo akiyafikiri lazima ajiulize nani alieviumba vyote hivi?

Nani alieiteremsha mvua kutoka mbinguni, ambayo uhai haupatikani isipokuwa kwayo, kwa mvua ameotesha mimea, miti, maua, matunda, na watu na wanyama wanapata maji, na akaiandaa ardhi kuhifadhi maji yake. Nani alieuweka kwenye Ardhi mvutano maalum kwa kiasi ya mahitaji ya vitu vilivyomo Ardhini, Hauzidi kuongezeka, kwa hivyo inakuwa ngumu kusonga juu yake, na haipungui kwa hivyo kufanya vitu havitulizani juu yake.

Nani aliemuumba mwanadamu kwa ubunifu wa hali ya juu, na kwa sura iliyo mzuri?

Na mtu akifikiri vizuri ataona maajabu makubwa katika ubunifu wa Muumba (Allah) na umadhubuti wa utengenezaji wake, fikiria viungo vya mwili

wako ambavyo vinafanya kazi kwa umadhubuti wa hali ya juu, na wala hatujui jinsi vinavyofanya kazi isipokua kwa uchache tu, na vipi utakuwa na uwezo wa kuvidhibiti?

Fikiria hewa unayoivuta, kama itasimama kwa muda mfupi tu utapoteza maisha, nani alieiweka?

Fikiria kuhusu maji unayokunywa, na chakula unachokula, na ardhi unayotembea juu yake, na pia mbingu na vilivyo mbinguni, na jua linalotupatia mwangaza, na mwezi na nyota na kila unachokiona kwa macho yako, nani alieviumba vyote hivyo?

Hakika huyo ni Allah. Allah ndie alieumba ulimwengu wote na yeye peke yake ndie anaeusimamia na kuuendesha.

Yeye ndie mola wako mlezi aliekuumba, kukupa riziki, na ndiye anaekupa uhai, na kukufisha, na yeye ndie aliekufanya uwepo baada ya kuwa si lolote.

Baada ya kuyajua haya yote, hivi kuna yeyote mwenye akili anaeweza kudhani kwamba huu ulimwengu umeumbwa kwa mchezo tu, na kwamba watu wanazaliwa na kuishi kwa muda kisha wanakufa na ndio mwisho hakuna lingine tena!

Kwa hivyo uhakika wa mambo ni upi? Na kwa nini tumeumbwa?

# KWA NINI TUMEUMBWA?

Allah ametuumba tumuabudu yeye peke yake, na akawatuma kwetu Mitume (wajumbe wake) na akatuteremshia vitabu, ili kufafanua vipi tumuabudu yeye? Kwa hivyo atakaemuabudu Allah na kutii amri zake na kuepuka makatazo yake, atapata radhi zake. Na asiemuabudu na akakataa kutii maamrisho yake atastahiki ghadhabu na adhabu yake.

Na Allah ameifanya hii dunia ni nyumba ya kufanya matendo na kujaribiwa.

Kisha siku ya kiama Allah atawafufua watu wote kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa. Na Allah ameandaa huko pepo yenye neema nyingi zisizowahi kuonwa na jicho la mtu yeyote, wala kusikiwa na sikio lolote, wala kuhisiwa na moyo wa mtu yeyote (hapa duniani). Hizi neema ameziandaa Allah kwa waumini ambao wamemuamini na kutii amri zake.

Na akaandaa moto ambao ndani yake kuna kila aina za adhabu ambazo hazijawahi kufikirika katika akili ya mtu yeyote, moto huu ameundaa Allah kwa kila aliempinga, na akamuabudu asiekuwa yeye, na kufuata dini isiyo ya Uislam.

## NI NINI UISLAM?

Uislam ndio dini aliyoichagua Allah, unamtaka mtu amuabudu yeye peke yake na kumtii mtume wake Muhammad- Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake.

Na hatomkubalia Allah mtu yeyote mwenye kufuata dini isiyokuwa ya kiislam, na Uislam si dini maalum kwa baadhi ya watu tu, bali ndio dini ya watu wote.

Na amewaamrisha Allah waja wake amri nyingi, na amewakataza mambo ya haram, atakaemtii atafaulu, na atakemuasi ataangamia na kupata hasara.

Na Uislam sio dini mpya, bali ni dini aliyowachagulia Allah waja wake tokea aumbe hii dunia, na ndio dini iliyolinganiwa na mitume wake wote- Rehema na amani ziwe juu yao.

## KISA CHA KUUMBA.

Kisa cha kuumba kilianza pale Allah alipomuumba baba yetu Adam -Amani iwe juu yake- pale alipomuumba kwa udongo, kisha akaupulizia roho, na kumfundisha majina ya vitu vyote, na akawaamrisha Malaika wamsujudie, ikiwa ni kumkirimu na kumtukuza zaidi, wakamsujudia wote

isipokuwa Iblisi alifanya kiburi na kukataa kwa kumfanyia hasadi Adam, Mwenyezi Mungu akamshusha kutoka mbimbuni na kumtoa hali ya kuwa dhalili na myonge, na akamhukumia kumlaani na maisha mabaya na moto.

Hakika Iblis aliomba kwa mola wake mlezi amsubirishe mpaka siku ya kiama, akamkubalia, na akaapa kuwa atahakikisha anawapotosha wana wa Adamu wote, na kuwaondoa kwenye njia iliyo sahihi (Uislam).

Kisha baada ya hapo Allah akamuumba mkewe Hawaa, ili apate utulivu na kilewazo kwake, na akawaamrisha wakae peponi, ambamo kuna kila aina ya neema, isiyopata kuhisiwa na mtu yeyote hapa duniani. Na Allah akawaeleza juu ya uadui wa Iblisi kwao, na akawakataza wasile mti Fulani ulio humo peponi, kama kuwajaribu na kuwapa mtihani, lakini Shetani akawatia ushawishi na kuwapambia kuula mti ule, na akaapa kwao kuwa yeye ni mshauri mzuri, na akawaambia; (ikiwa mtakula mti huu mtakuwa ni wenye kuishi milele).

Basi hakuacha kuwashawishi mpaka akafaulu kuwapotosha, wakala tunda la ule mti na kumuasi Allah mlezi wao. Na walipoligundua hilo walijuta

sana kwa tendo lao hilo, na wakatubia kwa mola wao mlezi, na mola wao akawakubalia toba yao. Lakini aliwashusha kutoka peponi na kuwaweka ardhini, na akaishi Adam na mkewe Hawaa Ardhini, na wakajaaliwa kizazi ambacho kiliongezeka kwa wingi mpaka kufikia hii leo.

Na bado Iblis na kizazi chake wanendeleza vita dhidi ya wanadamu, ili wawazuie kufuata uongofu, na kuwanyima kheri, na kuwapambia shari, na kuwaweka mbali na yale anayoyaridhia Allah, ikiwa ni pupa yake ya kutaka kuwaingiza motoni siku ya mwisho (Kiama).

Lakini Allah mtukufu hakuwaacha viumbe wake hivi hivi, bali aliwatumia Mitume ambao wanawabainishia haki, na kuwaelekeza kwenye yale yenye ufaulu kwao.

Alipokufa Adam kizazi chake kiliishi baadae kwa muda wa karne kumi, hali ya kuwa wao wanamtii Allah na kumpwekesha, kisha ukatokea ushirikina, na akaabudiwa asiyekuwa Allah pamoja na Allah, watu wakaanza kuabudu masanamu, hapo Allah akatuma Mtume wake wa kwanza ambae ni nabii Nuhu –Amani iwe juu yake- akiwaita

(kuwalingania) watu kumuabudu Allah peke yake na kuacha kuabudu Masanamu.

Kisha ikafululiza Mitume baada ya Nabii Nuhu, wakiwaita watu kwenye kuufuata Uislam, ambao ni kumuabudu Allah peke yake na kuacha kuabudu chochote kinyume na yeye.

Kisha akaja Nabii Ibrahim –Amani iwe juu yake- akawalingania watu wake kuacha kuabudu masanamu, na wamwabudu Allah pekee.

Na utume baada ya Nabii Ibrahim ni kwa watoto wake Ismaili, Is-haka, kisha kizazi cha Is-haka.

Na katika Mitume wakubwa katika kizazi cha Is-haka ni Yakobo, Yusufu, Musa, Daudi, Suleimani na Issa- Amani iwe juu yao-. Na baada ya Issa hapakuwa na mtume aliyetokana na kizazi cha Is-haka.

Baada ya hapo utume ulielekea kwa kizazi cha Ismail, pale alipomchagua Allah mtukufu Muhammad –Amani iwe juu yake- awe Nabii na mtume wa mwisho, na ujumbe wake ndio wa mwisho, na kitabu chake ndicho cha mwisho, ambacho ni Qur-an, ujumbe wa mwisho kwa mwanadamu kutoka kwa Allah.

Na ndio maana ujumbe wake umeenea, umekamilika, ni kwa watu wote na majini, kwa waarabu na wasio waarabu, ni wenye kufanya kazi zama zote, sehemu yeyote na jamii yeyote, na kwa hali zote, hakuna kheri isipokuwa umeielekeza, wala shari isipokuwa umeitahadharisha.

Na Allah hatamkubalia mtu yeyote kufuata dini yeyote isipokuwa dini aliyokuja nayo mtume Muhammad –Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-.

## MTUME MUHAMMAD- REHEMA NA AMANI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE:

Kwa hakika Allah amemtuma Muhammad - Rehema na Amani Za Allah ziwe juu yake -akamfanya yeye kuwa mtume wa mwisho na akaufanya ujumbe wake kuwa ujumbe wa mwisho.

Allah amemtuma mtume Muhammad - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - ili awaongoze watu kumuabudu Allah peke yake na kuacha kumuabudu asiekua Allah kama Masanamu, Mizimu na vinginevyo.

Amepewa utume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwa na umri wa miaka Arobaini katika mji mtukufu wa Makka.

Na alikua mtume Muhammad- Rehema na amani za Allah ziwe juu yake -ni mwenye kusifika na tabia njema katika jamii yake, kama vile ukweli, uaminifu, adabu za hali ya juu, mpaka jamaa zake wakampa jina na kummuita Muaminifu.

Alikua hasomi wala haandiki (Ummiyu), Allah akamfunulia Qur-an tukufu ambayo wameshindwa kuileta mfano wake viumbe vyote.

## UFUPISHO JUU YA NASABA YAKE NA MAISHA YAKE -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-:

Yeye ni Muhammad mtoto wa Abdallah mtoto wa Abdul- Mutwalib mtoto wa Hashim, anaetokana na kizazi cha Ismaili mtoto wa Ibrahim –Amani iwe juu yao -

Na mama yake ni Amina mtoto wa Wahabi mtoto wa Abdul Manafi mtoto Zuhrah, na Zuhrah ni ndugu wa babu yake Mtume -Reheme na amani za Allah ziwe juu yake.

Na Abdullah alimuoa mama yake mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake, na akaishi pamoja nae kwa muda wa siku tatu, na hakukaa muda mrefu akapata uja uzito wa Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- na hakupata kama ilivyozoeleka kwa wanawake wajawazito.

Na alizaliwa Mtume Muhammad- Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwa na sura nzuri na mwili uliosalama usio na kasoro yeyote, na kuzaliwa kwake ilikuwa mwaka mia tano na sabini na moja (571) Miladiya.

Na alifariki baba yake kabla ya kuzaliwa kwake, na aliesimamia malezi yake Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - ni babu yake Abdul - Mutwalib, na alinyonyeshwa na mama yake kwa muda wa siku tatu, kisha akanyonyeshwa na Halima Saadiya, aliekua anaishi kijijini (pembezoni mwa mji wa Makka).

Na ilikua desturi ya Waarabu kuwapeleka watoto wao vijijini kwa ajili ya kunyonya.

Kwa kuwa huko kijijini zinapatikana kwa wingi sababu za kukua kimwili katika afya njema.

Kwa hakika Halima Saadiya aliona maajabu pale tu alipoanza kumyonyesha Mtume- Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - na miongoni mwa hayo maajabu, hakika Halima Saadiya alifika mji wa Makka pamoja na mumewe akiwa na Ngamia aliekonda asieweza kutembea vizuri.

Na alipokua akirudi hali ya kuwa amemuweka Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- juu ya mapaja yake wakiwa juu ya Ngamia, basi akawa huyu Ngamia anakimbia kwa kasi, akiwaacha nyuma wanyama wote aliekua amefatana nao, jambo ambalo liliwafanya watu njiani washangae sana.

Kama alivyosimulia Halima hakika chuchu zake si zenye kutoa maziwa isipokua machache, na hakika mtoto wake aliekua akimnyonyesha kabla ya kuja Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alikua ni mwenye kulia muda wote kutokana na njaa. pindi alipoanza tu kumnyonyesha Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- yalianza kutoka maziwa mengi.

Na amesimulia kuwa kulikua na ukame katika miji ya Saadi, pindi tu alipofika Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- hali ikabadilika

kutoka kwenye ukame kwenda kwenye hali nzuri, kutoka kwenye ugumu kwenda kwenye wepesi.

Aliishi Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwa ni mwenye kulelelewa na Halima kwa muda wa miaka miwili, na alikua na hima katika kumlea kwake, na aliona vitu vingi na hali zisizo za kawaida kwa mtoto huyo.

Na baada ya hii miaka miwili Halima alimpeleka Mtume kwa mama yake na babu yake katika mji wa Makka, lakini Halima ambae aliona Baraka za Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ambazo zilimuathiri, hivyo akamsisitiza Mama yake mtume Bi Amina akubali abaki nae kwa mara ya pili, na Bi Amina akakubali maombi yake.

Na hivyo Halima akarejea nyumbani kwa Bani Saadi akiwa pamoja nae mtoto yatima (Muhammad), akiwa na utulivu na furaha tele.

Na baada ya miaka miwili Halima alimrejesha kwa mama yake kwa mara ya pili, na umri wa Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ukiwa ni miaka minne, akalelewa na mama yake mpaka alipofariki (mama yake), akiwa na umri wa miaka sita, baada ya hapo alilelewa na babu yake

Abdul- Mutwalib kwa muda wa miaka miwili kisha akafariki, kisha akalelewa na Ami yake Abuu Twalib na akamlea vizuri kama alivyokua akiwalea watoto wake, isipokua yeye alikua fakiri.

Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- hakuzoea maisha mazuri na ya starehe kwa hakika alizoea Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kuchunga Mbuzi na Kondoo pamoja na ndugu zake wa kunyonya katika kijiji cha Bani Saadi, hivyo basi akawa anachunga mbuzi wa watu wa Makka. Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akawa anampa baba yake mdogo kile anachokipata katika malipo.

Kisha alisafiri Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- na baba yake mdogo kuelekea Shamu kibiashara akiwa na umri wa mika kumi na miwili, kisha akasafiri kwa mara ya pili akiwa ni mwenye kufanya biashara ya Bi Khadija mtoto wa Khuwaylid, alikua ni mwanamke tajiri katika wanawake wa makka, Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-akapewa malipo makubwa tofauti na watu wengine kwa kuwa alirejea na faida kubwa.

Na alishirikiana katika msafara wa kibiashara kuelekea Shamu, ambayo Bi Khadija alichangia mali nyingi katika hiyo biashara, na huyu Bi Khadija ni mjane na tajiri,na alikuwa msimamizi wa mali zake katika msafara huo ni kijana wake Maisara, na kwa sababu ya baraka za Mtume na uaminifu wake ilipata biashara ya Bi Khadija faida kubwa ambayo haijawahi kutokea huko nyuma, akamuuliza kijana wake Maisara sababu ya kupatikana faida hii kubwa, akamwabia kwamba Muhammad Mtoto wa Abdillah ndie alisimamia kuuza, watu wakajitokeza kwa wingi na hivyo kupata faida kubwa bila ya kudhulumu, alimsikiliza Khadija kijana wake Maisara na alikuwa akijua baadhi ya mambo kuhusu Muhammad akazidi kupendezwa nae, akapenda aolewe nae, akamtuma mmoja wa watu wake wa karibu kwa ajili ya kumfikishia Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake– ili kupata mtazamo wa Mtume katika jambo hilo, na wakati huo Mtume alikuwa na umri wa miaka Ishirini na mitano, akafikiwa na huyu mwamke akimwelezea kuhusu mahitaji ya Bi Khadija ya kuolewa nae, akaridhia Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ndoa ikapita na kila mmoja alimfurahia na kumridhia mwenzake, akawa Muhammad sasa ndie

anaeongoza biashara za Bi Khadija, na akathibitisha uwezo wake wa kuongoza.

Na ikapita miaka kadhaa, akazaa na khadija mfululizo mpaka akawa na watoto kadhaa wa kike ambao ni Zainabu, Ruqaiya, Ummu kuluthum na Fatuma, na watoto wa kiume ni wawili Kasimu na Abdallah na hawa wakiume walifariki wakiwa wadogo.

Na pindi ulipokaribia umri wake miaka Arobaini alipenda kujitenga katika eneo la pango la Hiraa, kwenye mlima unaopatikana mashariki mwa mji wa Makka, akikaa humo siku kadhaa mfululizo akiwa anamuabudu Allah.

Na katika usiku wa tarehe Ishirini na moja katika mwezi wa Ramadhani,na akiwa katika hili pango, Na umri wake ukiwa umefika miaka Arobaini, alijiwa na Malaika Jibrili -Amani iwe juu yake- akiwa hapo kwenye pango la Hiraa, akamwambia Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : Soma, akajibu: mimi si msomi, (akiwa anakusudia kuwa hawezi kusoma), Akarejea tena Jibril kumtaka asome kwa mara ya pili na ya tatu,na katika mara ya tatu ndipo alipomwambia: "**Soma (Ewe Nabii) ukianza kwa**

**jina la mola wako aliepwekeka kwa kuumba (1) Alieumba kila binadamu kwa pande la damu mzito myekundu (2) Soma ( ewe Nabii) na mola wako ni mwingi wa ukarimu (3) Aliewafundisha viumbe vyake kuandika kwa Kalamu (4) Alimfundisha binadamu vitu ambavyo hakuwa akivijua (5)**” [Al-Alaq].

Kisha Jibrili akaondoka na kumuacha mtume, lakini Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- hakuweza kuvumilia kubaki pale pangoni, akarudi nyumbani kwake, na akaingia kwa mkewe Bi Khadija hali ya kuwa anatetema kwa hofu, na akasema**: ”nifunikeni nifunikeni”** wakamfunika mpaka ilipoisha hofu, hapo ndipo akamsimulia Bi khadija kile kilichomkuta na akamwambia:” **Hakika nilipata hofu katika Nafsi yangu**” na Bi khadija akamwambia: Naapa kwa Allah kamwe hatokufedhehesha, na utamsaidia Yule asiejiweza, na utamsaidia Fakiri, utamkirimu mgeni, na utasaidia kwenye matatizo ya dunia.

Na Baada ya kipindi kifupi Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alirejea tena katika pango la Hiraa, ili aendelee kumuabudu Allah.alipomaliza ibada yake alitoka pangoni ili arejee Makka , na alipokuwa katikati ya Bonde,

alimjia Malaika Jibril akiwa amekaa kwenye kiti , kati ya mbingu na Ardhi, na akamteremshia Wahyi (Ufunuo): " **Ewe uliojifunika nguo zako (1) Inuka kutoka kwenye malazi yako uwaonye watu ( na adhabu ya Allah) (2) Na umkusudie mola wako peke yake kwa kumtukuza (3) Na usafishe nguo zako kutokana na Najisi (4) na uendelee daima kuwa mbali na ushirikina (5)"** [Al-Mudathir].

kisha uliendelea mfululizo kushuka Ufunuo kwa Mtume mpaka alipofariki.

Na Allah alimuamrisha Mtume Muhammad - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- awalinganie watu juu ya kumuabudu Allah peke yake, na kuingia katika dini ya uislamu, Dini ambayo ameiridhia Allah kwa watu, na Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akawa anawalingania watu kwa hekima na kwa mawaidha yaliyo mazuri.

Na wa mwanzo kabisa kumuamini ni mke wake Bi Khadija, na katika watu wazima ni rafiki yake Abubakar Al–Swidiq, na katika watoto ni mtoto wa Ami yake Ally Bin Abi Twalib, kisha wakafululiza watu kuingia katika dini ya Allah, yakazidi maudhi ya washirikina kwa Mtume -Rehema na Amani za

Allah ziwe juu yake-, na akawa ni mwenye kuendelea kuwalingania watu pale Makka kwa kipindi cha miaka kumi na mitatu, na yakazidi maudhi ya washirikina kwake yeye na Maswahaba (wafuasi) wake, na akahamia yeye pamoja na Maswahaba wake kuelekea Madina, na huko aliendelea kulingania kuufuata Uislam, na baada ya kupita miaka kadhaa alirejea katika mji wa Makka na watu wake wote waliingia katika dini ya Uislamu.

Kisha alifariki Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwa na umri wa miaka sitini na mitatu, miaka Arobaini kabla ya utume na miaka Ishirini na mitatu ikiwa ndani ya Utume.

Na kwake mtume ndio Allah amekamilisha jumbe zake za mbinguni (Utume), na akalazimisha watu wote kumtii, na atakaemtii atapata maisha mazuri hapa duniani na ataingia peponi kesho Akhera, na atakaempinga atakuwa na maisha mabaya hapa duniani, na kesho Akhera ataingia motoni.

Na Allah alipomfisha Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- waliendeleza Wafuasi wake (Maswahaba) mwenendo wake, na kazi ya kulingania, na kueneza Uislam Duniani.

# MIONGONI MWA TABIA ZA MTUME MUHAMMAD -REHEMA NA AMANIA ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE-.

Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alisifika kwa tabia njema kabla ya Utume, na baada ya Utume tabia hizo ziliongezeka. Na hakika Allah amemzungumzisha katika Qur-an kwa kumwambia: "**Hakika wewe una tabia tukufu**" [Al Qalam,4.]

Na hakika alikua Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ni mfano wa kuigwa wa hali juu kwa mwenendo wake ulio mzuri kabla ya kupandikiza kile anachokisema kwenye miongoni hukumu na nasaha mbali mbali.

Kwa hakika Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alikuwa mfano wa hali ya juu kwa Maswahaba wake kwa tabia njema zile ambazo alikuwa akiwahimiza kuwa nazo, kwa hivyo alizipandikiza hizo tabia njema kwa maswahaba zake kwa kuzitenda yeye mwenyewe, kabla ya kuzihimiza kwa Maswahaba wake kwa maneno.

Kama alivyosimulia Swahaba Anas –Allah Amridhie– amesema:" **Nimemtumikia Mtume -**

**Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- muda wa miaka kumi, hakuwahi kuniambiakamwe: Wee, na wala hakuniambia kwa nini haukufanya hili, na kwa nini umefamya hili?**”.

Na anasimulia pia Anas -Radhi za Allah ziwe juu yake-: “nilkuwa nimefuatana na Mtume -Rehema za Allah ziwe juu yake- hali ya kuwa amevaa Joho zito, ghafla akajitokeza mwarabu Bedui akamvuta kwa nguvu, mpaka nikaona kwenye ngozi ya shingo ya mtume – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- athari za kule kuvutwa kwa nguvu, kisha akasema- Yule Bedui-: Wee Muhammad amrisha nipewe mimi katika mali za Allah ulizonazo! Nikageuka kumwangalia Mtume wa Allah, akacheka, na akaamrisha apewe chochote”.

Na Aliulizwa mama Aisha- Radhi za Allah ziwe juu yake- mke wa Mtume Muhamad - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake– kuhusu yale aliyokuwa akiyafanya Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake– akiwa nyumbani kwake? Akajibu: “**alikuwa akifanya kazi za nyumbani akiwasaidia wake zake, ukifika wakati wa swala hutawadha na kwenda kuswali** “.

Na anasimulia Abdallah Ibn Harith (Swahaba):” **Sijapatapo kumuona mtu yeyote mwenye**

**tabasamu sana kuliko alivyo Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake”**.

Na amesimulia Jabir –Allah amridhie- kuwa “**hajapatapo kuombwa chochote Mtume akakataa**”.

Na mambo linalotambulika kuwa katika tabia njema za Mtume -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake– kwamba alikuwa Mkarimu, Si Bakhili wa chochote kile, na alikuwa shuja kwenye kuitetea haki, alikuwa muadilifu katika kuhukumu, ahamdhulumu yoyote, alikuwa mkweli muaminifu kwenye maisha yake yote.

Na alikua ni mwenye utani kwa Maswahaba wake, na mwenye kuchanganyika nao, na alikua ni mwenye kucheza na watoto wao, na mwenye kuwakalisha katika mapaja yake, na alikua ni mwenye kuitikia mwaliko, mwenye kutembelea wagonjwa na mwenye kukubali dharura ya mwenye kutoa udhuru na alikua ni mwenye kuwaita Maswahaba waake kwa majina wanayoyapenda, na wala hayakati mazungumzo ya yeyote miongoni mwao.

Amesimulia Abu Qatada kuwa:” Pindi ulipokuja ugeni kutoka kwa mfalme Najashi, Mtume - Rehema

na amani za Allah ziwe juu yake - alisimama na kuwahudumia yeye mwenyewe, wakamwambia Maswahaba wake: sisi twakutosha, akasema Mtume: ‘’hakika wao walikuwa wakirimu kwa Maswahaba wetu nami napenda niwalipe kwa wema wao.’’

Na Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake – alikuwa akisema: ‘’**Hakika mimi ni mja nakula kama wanavyokula waja wengine, na ninakaa kama waja wengine, na alikua mtume - Rehema na amani za Allah ziwe juu yake- anapanda Punda na kuwatembelea masikini na wenye kukaa na mafakiri**.’’

Amesema mwana falsafa wa kiingereza Thomas Carlyle ambae alishinda zawadi ya Nobel, katika kitabu chake [Mashujaa] anasema:” kwa hakika ni aibu kubwa kwa mtu yeyote katika zama hizi kukubali kuwa dini ya uislamu ni ya uongo na Muhammad ni mzushi mwenye kudanganya.”

Na amesema Mwingereza Bernald show katika kitabu chake (Muhammad) amabacho kilichomwa moto na Utawala wa Uingereza:” Hakika ulimwengu unahitajia sana mtu mwenye fikra na busara kama Muhammad na dini yake aliyokuja nayo, huyu Mtume ambae ameifanya dini yake wakati wowte ni yenye kuheshimika na kutukuzwa, hakika dini hiyo

ndio yenye nguvu zaidi kulioko dini zote katika kuondoa matatizo, ni dini itakayobaki milele, na mimi nimewaona wengi katika watu wangu wameingia katika hii dini kwa ubainifu, na dini hii itapata nafasi kubwa katika bara la Ulaya”.

Na anaendelea kusimulia:” Hakika viongozi wa dini katika karne za kati, kwa sababu ya ujinga na ubaguzi, waliipa dini ya Muhammad sura mbaya, waliizingatia kuwa ni dini adui kwa Ukristo, lakini mimi nimechunguza mtu huyu nikamuona ni mtu wa ajabu sana, nikajua kuwa si adui wa Ukristo, bali anapasa aitwe ni mwokozi wa watu, na kwa rai yangu hakika mtu huyu kama angetawala ulimwengu leo, angewezesha kuondoa matatizo yote, na kueneza Amani na usalama amabyo wanaihitajia sana watu”.

## MIONGONI MWA MIUJIZA YA MTUME

### -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-:

Hakika muujiza mkubwa wa Mtume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ni Qur-an ambayo wameshindwa wanafasihi wote duniani kuleta mfano wake, na kuwapa changamoto viumbe wote duniani kuileta mfano wake, na wamekiri Makafiri kuwa wameshindwa.

Muujiza wa pili ni kupasuka kwa mwezi pale alipopewa mtihani na makafiri wa makka na kisha ukarejea katika hali yake.

Muujiza wa tatu ni kutoka katika vidole vyake na vikamtakasa vijiwe vya changalawe katika mkono wake.

Muujiza mwingine ni muarabu wa mashambani alimuomba Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake amuoneshe alama za utume wake, Mtume akauamrisha mti ukaja kwake na kurudi sehem yake.

Pia alishika chuchu za maziwa ya mbuzi ambae hatoi maziwa na akazifuta kisha akakamua maziwa akanywa na akampa rafiki yake Abuu bakari.

Pia Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake alimtemea Ally mate machoni kisha akapona ugonjwa wake muda ule ule.

Na pia auliumia mguu wa mmoja wa Maswahaba, na Mtume akaushika na kuufutafuta ukapona mda huo huo.

Pia alimuombea Anasi awe na umri mrefu, mali nyingi, watoto wengi, na allah ambariki katika hayo, akapata watoto mia na Ishirini, na akawa na shamba

la mitende, ambalo alikuwa akivuna mara mbili kwa mwaka, na katika hali kawaida Mitende huzaa mara moja tu kwa mwaka, na yeye akaishi miaka mia moja na Ishirini.

Pia mmoja ya maswahaba alimlalamikia Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kuwa kuna ukame hali ya kuwa Mtume akiwa juu ya Mimbari, Mtume akamuomba Allah, na hapakuwa na mawingu ya mvua mbinguni, yakajikusanya mawingu mengi mfano wa majabali, na ikanyesha mvua nyingi kwa muda wa wiki mzima, wakamlalamikia kuwa sasa mvua imekuwa nyingi mno, ndipo Mtume akamuomba Allah kwa mara ya pili, na mvua ikaacha kunyesha.

Miongoni mwa miujiza ya Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ni kwamba aliwalisha watu walioshiriki vita vya Handaki, ambao idadi yao ni Elfu moja, pishi moja ya Shairi na mbuzi mmoja, wakala na wakashiba na kuondoka, hali ya kuwa chakula kilibaki vile vile bila ya kupungua hata kidogo.

Na pia katika Miujiza yake, ni kuwa alitoka nje ya nyumba yake hali ya kuwa makafiri wameizingira,

kwa lengo la kumuua, akawamwagia mchanga machoni kisha kuondoka na hawakuweza kumuona.

Na pia katika Miujiza yake ni kuwa alifuatiliwa na bwana mmoja aitwae Suraqa Bin Maliki ili amuue, na alipomkaribia, Mtume alimuombea dua baya, ikazama ardhini miguu ya Farasi wake.

Na miujiza ya Mtume Muhammad -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake- ni mingi mno, na yote inatoka kwa Allah –Mtukufu- kwa lengo la kutilia nguvu ukweli wa ujumbe wake.

## MISINGI YA DINI YA KIISLAM

**1- Kumuamini Allah:** Hii ni asili ya dini ya kiislam, na ndio Imani ya kumuamini Allah, na kumsadikisha kwa uwepo wake, na kwamba Allah ndio muumba wa kila kitu na yeye peke yake ndio mwenye kuupangilia ulimwengu wote, naye ndio anaestahiki kuabudiwa bila ya kushirikishwa na yeyote, na yakwamba Allah ni mwenye kusifika na kila sifa ya ukamilifu na ametakasika na kila aina ya aibu na mapungufu, na kwamba hafanani na kiumbe yeyote yule.

Na kwa yeyote atakae angalia ulimwengu na akaangalia vilivyomo, basi atatambua kuwa haiwezekani hivi vitu kujiumba vyenyewe, na haiwezekani vipatikane bila muumba, bali muumba wa vyote hivyo ni Allah.

**2- Kuamini Malaika:** Malaika ni ulimwengu wa ghaib (visivyo onekana) wameumbwa kwa kutekeleza Ibada tu, hawahusiki na mambo ya uumbaji wala kuabudiwa, Allah amewafanya wawe na utekelezaji wa amri zake, na uwezo wa kutekeleza bila kuasi.

Na muislam anatakiwa kuamini kuwepo kwao, na kwamba malaika wako wengi, hakuna anaejua idadi yao ispokuwa Allah tu.

Pia kuyaamini majina ya wale tuliofundishwa majina yao, kama vile: Jibril, Maliki, Mikail, na wengineo.

Pia kuziamini sifa zao na matendo yao tuliyofundishwa.

**3- Kuviamini Vitabu:** Muislamu anatakiwa aamini yakwamba Allah –Alietakasika na mapungufu- ameteremsha vitabu kwa baadhi ya Mitume na Manabii wake, kwa lengo la kubainisha haki na

kuilingania, Mfano: Taurati kwa Nabii Mussa, Injili kwa Nabii Issa, Zaburi kwa Nabii Daudi, na kuiamini Qur-ani ambayo Allah aliiteremsha kwa Mtume wake wa mwisho Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-.

**Qur-an**: Huu ni ujumbe wa Allah alioutuma mwisho kwa ajili ya wanaadamu, na Allah hatokubali matendo ya mmoja wenu isipokuwa kwa kufuata kilichokuja ndani ya Qur-an, na Qur-an hii imekuja kutia nguvu Vitabu vilivyotangulia na kuvisadikisha, pia kinapambanuka kitabu hiki yakwamba Allah ameahidi kukihifadhi na kukilinda, hakiingii dosari wala mabadiliko, hii inaenda tofauti na Vitabu vilivyotangulia, ambavyo vilibadilishwa, ni kwa sababu tu kwamba Allah hakuahidi kuvilinda na kuvihifadhi kama ilivyo kwenye Qur-an.

Qur-an katika us-lub (muundo) wake kilugha, ipo katika sura nzuri zaidi, na katika upande wa sheria kuna kanuni iliyo kamilika zaidi, na katika mambo ya kiibada na kuelezea mambo ya ghaib (yasiyo julikana), imetuletea vile ambavyo hakuna mwanadamu anaevifahamu, na wala haiwezekani kwa akili ya mmoja yeyote akaweza kutambua, na Qur-an kwa tabia yake huwa inaashiria kwenye kanuni ambazo hakukuwa na mmoja yeyote katika

zama za Mtume Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake- akizifaham, na wala zama zilizofuata ambazo zilikuja baada ya Mtume Muhammad, ndani ya Qur-an kuna ishara ya kanuni ambazo hazikugunduliwa ila baada ya kufa kwa Mtume Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake- kwa miaka 1300, na kuna nyingine hazijagunduliwa hadi sasa.

Qur-an ni kitabu ambacho Allah aliwatambia watu kwa kuwapa changamoto, kwa walete- iwapo wataweza- sura kumi mfano wa Qur-an au walete sura moja tu nao wakashindwa, na hali hiyo inaendelea mpaka sasa na wataendelea kushindwa.

Miujiza ya Qur-an bado ipo na hii si kwenye maneno tu na wala sio kwasababu ya kuelezea yasiyo julikana, au kwasababu ya mpangilio wa sheria tu, bali Qur-an yote ni miujiza.

**4- Kuwaamini mitume:** Muislam anatakiwa kuamini yakwamba Allah aliwatuma kwa lengo la kuwaambia wanaadamu kuwa wamuabudu yeye peke yake, na kukiacha kila kinachokwenda kinyume na hilo.

Na kwamba Mitume ni wanaadamu walioumbwa na wala hawahusiki kwenye uumbaji wala kuabudiwa,

sifa yao ni kuwa binaadamu wa kawaida ambao wanakula, kunywa, kuugua, na kufa.

Mitume ni viumbe bora ambao Allah aliwachagua na akawahusisha wao tu kuwapa ujumbe.

Kuwaamini mitume ni pamoja na kuamini walichokuja nacho kutoka kwa Allah kuwa ni kweli, pamoja na kuamini majina yao kwa wale tuliofundishwa kwa majina, na kusadikisha maelezo yao kisha kuifanyia kazi sheria na muongozo uliokuja na wa mwisho wao Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake- kwani Allah hakubali sheria ya Mtume mwingine yeyote yule.

**5- Kuamini siku ya mwisho:** Nayo ni siku ya Qiyaama, ambapo Allah atawafufua watu wote kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa, imeitwa siku ya mwisho kwakuwa hakutakuwa na siku nyingine baada ya hiyo, hapo ndipo watu wa peponi watakaa majumbani mwao na watu wa motoni nao watakaa majumbani mwao.

Maana ya kuiamini siku ya mwisho ni kwamba, kusadikisha kusiokuwa na shaka juu ya kuja kwake, na kulifanyia kazi hilo, na hii inakusanya mambo matatu:

a) Kuamini kufufuliwa, nako ni kuwafufua waliokufa, pale Allah atawafufua watu wote waje wasimame kutoka makaburini mwao wakiwa bila nguo, bila viatu, na bila kufanyiwa twahara (kutahiriwa).
b) Kuamini kulipwa na kuhesabiwa, ambapo Allah atamuhesabia kila mwanaadamu juu ya matendo yake aliyoyafanya hapa duniani, na amlipe kila mmoja, alie amini na kutenda mema amlipe pepo na alie kufuru na kutenda maovu amlipe moto.
Malipo na hisabu ni kwa mujibu wa hekma ya Allah kwa waja wake, kwani Allah aliteremsha Vitabu na kutuma Mitume wakiwabainishia watu kheri na shari, na akawajibisha kwa wanaadamu kumuabudu na kumtii yeye peke yake.
Kisha hao wanaadamu wako waumini na wengine ni makafiri, haiwezekani kwa uadilifu wa Allah na hekma yake hawa wawe sawa, amesema Allah –Mtukufu alietakasika na mapungufu- katika Qur-an: ‘’Hivi tuwafanye waislamu kama vile waovu (35) **mna nini nyie vipi mnahukumu (36)**”.
C) Kuamini pepo na moto, na kwamba hayo ni mafikio ya waja ya milele, pepo ni nyumba ya neema ambayo ameiandaa Allah kwa ajili ya waumini wachamungu, ambao wameyaamini yale

Allah aliwajibisha kwao, wakasimamia kumtii Allah na Mtume wake wakifanya Ibada kwa Ikhlasi na kwa kumfuata Mtume wake, na watu peponi watakua na madaraja tofauti, hii ni kwa kutofautiana kwao matendo mema.

Ama moto ni nyumba ya Adhabu ambayo ameiandaa Allah kwa makafiri ambao waliyakanusha na kuyapinga mafundisho ya Mitume wake, na watu wa motoni pia watakuwa na madaraja tofauti, kwa kutofautiana uovu wao.

**6- Kuiamini Qadari:** Hii ni kuamini mwanaadamu kwamba Allah anajua kilichopo kilichopita na kitachokuja, na akitakacho Allah kitakuwa na asicho kitaka hakiwezi kutokea, na kwamba hakitokei chochote kile ila kwa elimu yake (anakijua) na utashi wake.

# IBADA KATIKA UISLAMU

Haikubaliki ibada yoyote ile katika Uislamu isipokuwa itekelezwe kwa ajili ya Allah tu na iende sambamba na alichokuja nacho Mtume Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-

Swala kwa mfano, hii ni ibada ambayo haitekelezwi ila kwa ajili ya Allah, na haiwezi kuwa sahihi isipokuwa itekelezwe kwa kufuata utaratibu alioubainisha Mjumbe wa Allah -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-

Na hilo lina sababu zake, nazo ni:

1. Allah aliamrisha ibada itekelezwe kwa Ikhlasi ya kuabudiwa yeye tu, akiabudiwa mwingine pamoja na Allah huko ni kumshirikisha, Allah anasema: **"Muabuduni Allah na wala msimshirikishe na chochote kile"** [Nisaa 36].
2. Allah –Mtukufu alietakasika na mapungufu- ndie aliehusika kuweka sheria, kwahiyo ni haki yake peke yake, na atakae abudu kupitia sheria ambazo hakuziweka Allah huyo atakuwa amemshirikisha Allah kwenye uwekaji sheria.

3. Allah ametukamilishia dini, hivyo basi yule ataevumbua Ibada yake, huyu atakuwa ameituhumu dini kuwa ina mapungufu.
4. Lau ingekuwa kila binadamu inafaa kufanya ibada aitakayo kwa muundo autakao, basi kila mmoja angekuwa na utaratibu wake maalum wa kufanya ibada, kwa kule kutofautiana tabia na mienendo yao.

## NGUZO ZA UISLAMU

Nguzo za Uislamu ambazo Allah ameziamrisha ni tano:

1. Kushuhudia yakwamba hapana apasae kuabudiwa isipokuwa Allah na hakika Muhammad ni mjumbe wa Allah.
2. Kusimamisha Swala.
3. Kutoa Zaka.
4. Kufunga Ramadhani.
5. Kuhiji Nyumba ya Allah.

## Maana ya nguzo za Uislamu

1- Kushuhudia yakwamba hapana apasae kuabudiwa isipokuwa Allah na hakika Muhammad ni mjumbe wa Allah.

Maana ya shahada hii ni: Kushuhudia kwa kuitakidi bila ya kuwa na shaka na kutamka kwa ulimi, yakwamba Allah ndio muabudiwa wa haki yeye peke yake wala hana mshirika, na kushuhudia kwamba Muhammad ni mfikishaji wa ujumbe wa Allah.

Hautakubaliwa Uislamu wa mtu yeyote wala matendo yake ila kwa Ikhlas ya Allah na kumtii Mtume wake Muhammad -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-.

Maana ya –**Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah**- ni kutamka Mwanadamu huku akiitakidi kuwa Allah ndie mwenye haki ya kuabudiwa peke yake, na wala haitoshi kutamka tu, bali ni lazima kuambatane na matendo yanayofuata maamrisho ya Allah mtukufu.

Maana ya -Muhammad ni mjumbe wa Allah- ni kumtii kwa aliyoyaamrisha, kuyasadikisha aliyo yaeleza, na kujiepusha na yote aliyoyakataza na

kuyakemea, na asiabudiwe Allah ila kama alivyoelekeza.

2- Kusimamisha Swala: Swala za faradhi katika Uislamu ni tano kwa kila siku, ambazo ni: Al-Fajiri, Al-Adhuhuri, Al-Asiri, Al-Maghribi na Al-Ishaa.

3- Kutoa Zaka: Ni kutoa kiwango maalum cha mali kwa wanaostahiki, ambao ni Mafakiri wenye kuhitaji na wengineo.

Na katika faida ya Zaka ni: Kuitwaharisha nafsi kutokana na ubakhili, kukidhi haja za Waislamu wenye mahitaji, kueneza mapenzi kati ya waislamu, kuwa mbali na hasadi, kupata unyenyekevu na huruma na kuhisi shida za wengine.

4- Kufunga Ramadhani: Nayo ni kumuabudu Allah kwa kujizuia na vinavyofunguza katika mchana wa Ramadhani, nalo huwa kwa Muislamu kuacha kula kunywa kustarehe na mke/mume, na mfano wake kuacha vyote vinavyo funguza, kuanzia kuchomoza kwa Jua mpaka kuzama kwake, kwa muda wa mwezi mzima, ikiwa ni Ibada kwa ajili ya Allah.

Na katika faida ya Swaumu ni pamoja na: kuitakasa nafsi, kuizoesha kuacha vinavyopendeza, kwa lengo

la kumridhisha Allah, na kuizoesha nafsi Subira na kuvumilia hali ngumu.

Pia katika faida ni kukuza Ikhlas katika kutenda kwa ajili ya Allah, mtu kuwa mwaminifu, kuhisi shida za wengine na kupata afya njema ya Mwili.

5- Kuhiji Nyumba ya Allah: Nayo ni kumuabudu Allah kwa kuikusudia Nyumba yake tukufu iliyoko Makkah kwa lengo la kusimamisha alama (matendo) ya Hijjah, mara moja tu katika umri, kwa mwenye uwezo.

# MIONGONI MWA SIFA (MAALUM) ZA DINI YA UISLAMU

Uislamu ni Dini ambayo ameichagua Allah kwa ajili ya watu wote, ni Dini ambayo inafaa kwa kila zama na sehem yeyote ile, haijaacha jambo la kheri ila imelielezea na haikuacha jambo la shari ila imetahadharisha, na wanadamu kamwe hawawezi kupata raha wala kuishi maisha yenye utulivu ila wakiishi kwa kufuata Uislamu, na zile sifa maalum zilizopo katika Uislamu haziwezi kupatikana kwenye Madhehebu mengine wala kwenye Dini nyingine.

Na katika sifa maalum za Uislamu na ambazo watu wanazihitajia zaidi ni hizi zifuatazo:

1. Uislamu ni Dini iliyotoka kwa Allah, na Allah –mtukufu- ndie anaejua mambo yenye maslahi kwa waja wake, amese Allah -Mtukufu- **“Oh! Asijue alieumba! Na ndie avijuae visivyojulikana”** [Al-mulk: 14].
2. Uislamu unabainisha mwanzo wa mwanadamu na mwisho wake, na malengo ya kuumbwa kwake, na unamuwekea wazi njia ambayo anawajibika

kuifuata kwenye haya maisha, na unaweka wazi pia mambo ambayo atalazimika mwanadamu kujiepusha nayo na kuchukua tahadhari nayo.

Anasema Allah-Mtukufu- katika Qur-an **“Enyi watu! Muogopeni mola wenu ambae amekuumbeni kutokana na nafsi moja, na akaumba kutokana na hiyo nafsi mke wake, akaeneza kutokana na hao wanaume wengi na wanawake”** [Al-nisaa: 1], na amesema tena Allah –Mtukufu- **“Kutokana na udongo ndio mmeumbwa na katika udongo mtarudishwa, na kutoka hapo mtatolewa kwa mara nyingine”** [Twaha: 55], na akasema tena Allah –Mtukufu alietakasika na mapungufu- **“Sikuwaumba majini na wanadamu isipokuwa kwa lengo la kuniabudu”** [Al-dhariyat: 56], na amesema tena Allah –Mtukufu- **“Leo hii nimekamilisha kwenu dini yenu, na nimetiza juu yenu neema zangu, na nimeridhia kwenu Uislamu kuwa ni Dini”** [Al-maida: 3].

3. Dini inayoendana na maumbile, kwani haipingani na maumbile ambayo Allah aliyomuumbia mwanadamu, amesema Allah –Mtukufu alietakasika na mapungufu- **“Ndio umbile ambalo Allah amewaumbia watu”** [Al-roum: 30].

4. Dini ambayo inaihifadhi akili na inamuamrisha mwanadamu kufikiri, inapinga ujinga na kuiga hovyo, pia inapinga kuacha kufikiri fikra salama, amesema Allah –Mtukufu- "**Sema! Hivi wanalingana sawa wale wanaojua na wasiojua, wanaotanabahi hilo ni wale wenye akili tu**" [Al-zumar: 9], amesema tena Allah- **"Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja –za kuonyesha kuwapo mungu mmoja- kwa wenye akili (190) ambao humkumbuka Mwenyezi mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala, na huzingatia umbo la mbingu na ardhi –pia namna gani Mungu alivyoumba! Wakasema- Mola wetu! Hukuviumba hivi bure, utukufu ni wako basi tuepushe na adhabu ya moto"** [Aali-imran: 190-191].
5. Uislamu ni itikadi na sheria, umekamilika kiitikadi na kisheria, sio kwamba ni dini ya kufikiri tu, bali ni dini iliyokamilika kwa kila kitu kwenye maisha ya mwanadamu.

6. Dini inayozingatia hisia za kibinadamu, na kuzielekeza njia sahihi itayozifanya kuwa nyenzo za kujenga na si zakubomoa.
7. Ni Dini ya uadilifu, kwa kila mtu hata kama ni adui ama rafiki, jamaa wa karibu ama mbali, amesema Allah –Mtukufu- "**Hakika Allah anaamrisha uadilifu**" [Al-nahli: 90] akasema tena: "**Na msemapo –katika shahada na penginepo- kuweni na uadilifu ingawa ni jamaa"** [Al-an-aam: 152] na akasema tena: "**Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu, fanyeni uadilifu huko ndiko kunamkurubisha mtu na ucha-Mungu**" [Al-maida: 8].
8. Uislam ni dini yenye undugu wa kweli, Waislamu wote ni ndugu katika dini, hawatenganishwi na miji, utaifa, rangi, na wala hakuna ubinafsi kwa utaifa, rangi, wala familia, kipimo cha ubora kwa Muislamu ni Taqwa (uchamungu) amesema Allah –Mtukufu- "**Hakika ahishimiwae sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Munguni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi**" [Al-hujraat: 13]

9. Uislam ni dini ya elimu, inawaamrisha wafuasi wake kutafuta elimu na kuwaahidi malipo makubwa kwenye hilo, amesema Allah –Mtukufu-: "**Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu na wale waliopewa ilimu watapata daraja zaidi**" [Al-mujaadila: 11] akasema tena: "**Sema: Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?"** [Al-zumar: 9], na akasema Mjumbe wa Allah - Rehma na amani za Allah ziwe juu yake- "Kutafuta elimu ni faradhi (lazima) kwa kila Muislamu".
10. Allah amechukua dhamana kuwa kila mwenye kuufanyia kazi Uislamu kiusahihi basi ataishi maisha mazuri na maisha ya heshima, sawa sawa mmoja mmoja ama jamii kwa ujumla wake, amesema Allah –Mtukufu- "**Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao na kwa yakini atawasimamishia**

**Dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia Amani baada ya hofu yao, wawe wananiabudu hawanishirikishi na chochote**" [An-nur: 55] amesema tena: "**Mwenye kufanya matendo mema awe mwanaume au mwanamke ilihali ni muumini, tutampa maisha mazuri na tutawapa ujira wao mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda**" [An-nahli: 97].

11. Uislamu ni Dini ya upendo na yakijamii, kuzoeana na kuhurumiana, amesema Nabii: – Rehma na amani za Allah ziwe juu yake- "Mfano wa waumini katika kupendana upole na kuoneana kwao huruma ni sawa na mwili wa mtu mmoja, kikihisi maumivu kiungo kimoja husababisha mwili mzima kupata homa na kukesha" amesema tena: "Wale wenye kuwahurumia watu, nao watahurumiwa na Allah, waoneeni huruma waliopo Ardhini ili muonewe huruma na aliepo Mbinguni " akasemsa tena: "Hawi muumini wa kweli mmoja wenu hadi ampendelee ndugu yake kile anachokipendelea kwenye nafsi yake".

12. Uislamu ni Dini ya jitihada na kujituma, amesema Nabii: –Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake- “Muumini mwenye nguvu ni bora zaidi na mwenye kupendwa na Allah kuliko muumini dhaifu, pupia lenye manufaa na wewe na wala usishindwe, na ukipatwa na lolote usiseme: Lau ningefanya kitu kadhaa ingekuwa kadhaa, bali sema: Allah ndie aliekadiria na akitakacho hukifanya”.
13. Uislam uko mbali sana na mapungufu, amesema Allah –Mtukufu- “**Ingekuwa Qur-an imekuja kutoka kwa asiekuwa Allah, wangekuta humo tofauti nyngi**” [An-nisai: 82].
14. Uislamu uko wazi na mwepesi kuufahamu kwa kila mtu.
15. Uislamu uko wazi kwa kila anaetaka kuingia na kuusoma.
16. Uislamu unalingania tabia njema na matendo mema, amesema Allah –Mtukufu- “**Kubali kusamehe, amrisha mema, jiepushe na wajinga**”[Aaraaf: 199] amese tena: “**Mzuie kwa kufanya jambo jema, hivyo basi yule**

**aliyekuwa na uwadui kati yake na wewe atakuwa kama vile ni jamaa mwenye mapenzi na wewe**" [Fuswilat: 34], amesema Mtume –Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Yatayo waingiza watu peponi kwa wingi ni Taqwa ya Allah na tabia njema", amesema tena: "Mkamilifu wa watu kiimani ni mzuri wao kitabia" na akasema tena: "Anaependwa zaidi na Allah katika watu ni yule mwenye kuwanufaisha wenzie, na matendo yanayopendwa zaidi na Allah -Mshindi na mtukufu- ni furaha utakayo iingiza kwa Muislamu, au kumuondoshea tatizo, au kumlipia deni, au kumuondoshea njaa, na kwenda kutatua haja ya ndugu yangu Muislamu jambo hilo linapendeza zaidi kwangu kuliko kukaa itikafu Msikitini mwezi mzima".

17. Uislamu unahifadhi akili, ndio maana ukaharamisha pombe na dawa za kulevya, na kila kinachopelekea akili kuharibika, na kuua nafsi, amesema Allah –Mtukufu-: "**Msiziue nafsi zenu hakika Allah amekuwa mpole kwenu**" [An-nisai: 29]

18. Uislamu unahifadhi mali, ndio ukahimiza uaminifu kwa kuwasifu waaminifu na kuwaahidi maisha mazuri na kisha kuingia peponi, pia Uislamu umeharamisha wizi na kumuahidi atakaefanya hivyo adhabu hapa duniani na akhera, ili mtu asijihusishe kuiba mali za watu na kuwatia hofu.
19. Uislamu unahifadhi nafsi, ndio ukaharamisha kuua na kuweka adhabu ya kifo kwa muuaji, kisha kumuahidi kukaa motoni milele siku ya kiyama, kwa sababu hiyo ndio maana matukio ya mauaji yamekuwa machache kwenye miji ya Wasilamu ambayo inafanyia kazi sheria hizi, na pale anapofahamu mwanadamu kuwa akiua nae atauwawa, hapo atajizuia, na watu wataishi kwa raha bila shari za waovu.
20. Uislam unahifadhi afya, amesema Allah – Mtukufu-: "**Kuleni kunyweni wala msifanye israf, hakika yeye hawapendi wanaofanya israf**" [Aaraaf: 31] wamesema wanachuoni: "Hakika aya hii imekusanya kila aina ya tiba, na

jambo hilo nikwamba ukati na kati katika kula na kunywa ni katika sababu ya kulinda afya”.

Pia uislam umehifadhi afya kwa kuharamisha pombe na dawa za kulevya, na hilo halina kificho kuwa lina madhara mengi, kama ulivyoharamisha zinaa na liwaat, kwakuwa nayo yana madhara mengi yakiwemo madhara ya kifya kama vile: Kaswende, Gonoria, Malengelenge, na Ukimwi (Aids).

Uislamu umedhamini na kudhibiti uhuru wa binadamu, katika kuuza na kununua kwake, biashara na kusafiri kwake na mfano wa hayo muda wa kuwa hajavuka mipaka ya Allah katika ghushi, udanganyifu na uharibifu.

Mwanadam katika Uislamu yuko huru katika kunufaika na vitu vya halali kwenye maisha yake, vikiwemo vyakula vinywaji manukato na mavazi, muda wakuwa hajafanya mambo ya haramu au madhara yanayorudi kwake au kwa mwengine.

## MIONGONI MWA MAZURI YA UISLAMU

Umekuja Uislamu ili kumfundisha mwanadamu yale anayo yahitaji katika hii dunia, na yale ambayo yanakuwa ni sababu ya kuishi maisha mazuri ya hapa duniani na kesho akhera.

Na katika mambo mazuri kwenye Uislamu ambayo tunayapata kwa kuyaangalia maamrisho na makatazo ya Allah ni kama ifuatavyo:

a-**Maamrisho ya Uislamu**.

1) Uislamu unaamrisha kitu kitachoinua heshima ya mwanadamu kwa kujiepusha na kinachoshusha heshima yake, au kuwa mwenye kufuata matamanio yake, pia kuto kumtukuza asiekua Allah katika viumbe, na kuto mnyenyekea asiekua Mola wake.
2) Uislamu unaamrisha kutumia akili na viungo kwa kufanya ambayo ameumbiwa ikiwemo kutenda yatayoleta manufaa katika mambo ya dini na dunia.
3) Uislamu unaamrisha Ikhlas katika ibada ya Allah, na kuacha kumuabudia asiekua Allah katika viabudiwa vya batili.
4) Uislamu unahimiza kutatua haja za watu kwa kuwasaidia.
5) Uislamu unaamrisha kuwatembelea wagonjwa, kusindikiza Jeneza, kuzuru Makaburi na kuwaombea Dua Waislamu.

6) Uislamu unaamrisha kuwafanyia watu uadilifu, kutowadhulumu, na apende mtu kuwafanyia kile anachopenda kufanyiwa.
7) Uislamu unaamrisha kutafuta riziki, kuipa heshima nafsi yake, na kutoiingiza kila sehemu ya udhalili na kuomba omba.
8) Uislamu unaamrisha kuwafanyia viumbe huruma upole, kuwaangalia, kufanya yenye manufaa na wao, na kuwaondoshea madhara.
9) Uislamu unaamrisha kuwafanyia wema wazazi wawili, kuunga undugu, kumkirimu jirani na kuwafanyia upole wanyama.
10) Uislamu unaamrisha kuwatekelezea marafiki, na kuwa na muamala mzuri kwa mke/mume pamoja na watoto.
11) Uislamu unaamrisha uaminifu, kutekeleza ahadi, kuwa na dhana nzuri, na kufanya mambo kwa upole, na kuharakisha kufanya mambo ya kheri.

## Na yasiyokuwa hayo katika maamrisho mazuri ya Allah.

### b-Makatazo katika Uislamu.

Na katika mambo mazuri kwenye Uislamu ni yale yaliyoletwa na Uislamu yakiwemo makatazo yake ambayo yanamtahadharisha Muislamu kutoingia katika mambo ya shari, na kumuonya na mwisho mbaya, ambao asili yake matendo mabaya, ili wanadamu wote waishi kwa Amani, na katika mambo ambayo Uislamu umekataza ni haya yafuatayo:

1) Uislamu umekataza ukafiri na ushirikina.
2) Umekataza kiburi, chuki, kujiona, husda na kufurahia matatizo ya wengine.
3) Umekataza dhana mbaya, kuhisi nuksi, kukata tamaa, ubakhili na kufanya is-raf.
4) Umekataza uvivu, uoga, udhaifu, kutofanya kazi, uharaka, lugha chafu, uchache wa haya, kukosa subira, uzembe, hasira, kutokuwa na busara, kukasirishwa na jambo lilichopita.
5) Umekataza ukaidi, na kuwa na rohombaya kiasi cha kutowasaidia wenye shida.

6) Umekataza kusengenya, ambapo ni kuwazungumza watu kwa yale yanayo wachukiza, pia umekataza umbea, ambao ni kuhamisha maneno kwa watu kwa lengo la kuharibu.
7) Umekataza maneno mengi yasiyokuwa na faida, pia kutoa siri, kuwadhalilisha watu na kuwadharau wengine.
8) Umekataza kutukana kulaani na kuitana majina mabaya.
9) Umekaza mijadala, ugomvi, na utani mbaya ambao unapelekea kwenye shari.
10) Umekataza kuficha ushahidi, ushahidi wa uongo, kuwazushia wanawake wema mambo machafu, kuwatukana wafu na kuficha elimu.
11) Umekataza upuuzi, maneno mabaya, kusimbulia katika kutoa sadaka, na kutomshukuru aliekufanyia wema.
12) Umekataza hiyana vitimbi na kutotekeleza ahadi.
13) Umekataza kutowaheshimu wazazi, kuvunja undugu, na kuwapuuzia malezi ya watoto.

14) Umekataza kufuatilia aibu za watu.

15) Umekataza wanaume kujifananisha na wanawake na wanawake kujifananisha na wanaume.

16) Umekataza kunywa pombe, kutumia madawa ya kulevya, na kucheza Kamari ambavyo vinaharibu mali.

17) Umekataza kuzipamba bidhaa kwa viapo vya uongo, kupunguza vipimo, kutoa mali kwa njia za haramu na kumuudhi jirani.

18) Umekataza kuiba kupora kufanya hiyana kwa walio shirikiana, kuchelewesha malipo kwa mwajiriwa pamoja na kutomlipa baada ya kumaliza kazi.

19) Umekataza kula sana kiasi cha mtu kupata madhara.

20) Umekataza kutengana, kugombana, na kufanyiana uadui, pia umehadharisha Muislamu kumtenga ndugu yake zaidi ya siku tatu.

21) Umekataza kumpiga mtu bila sababu ya kisheria, na kuwatishia watu kwa silaha.

22) Umekataza zinaa, kulawiti, na kuua nafsi isiyo na hatia.
23) Umekataza kuchukua rushwa na kutoa pia.
24) Umekataza kutomsaidia aliedhulumiwa kwa yule mwenye uwezo wa kumsaidia.
25) Umekataza mtu kuangalia kwenye nyumba ya mwenzie bila idhini yake, na kusikiliza mazungumzo ya watu wasiopenda ayasikie.

## SIKU YA MWISHO

Hawi mwanadamu muumini wa kweli mpaka aamini siku ya mwisho na yale yanayohusiana na siku hiyo, ambayo Allah amesema: "**Siku ambayo huwafanya watoto wadogo watokwe na mvi**" [Muzammil: 17] na katika hayo mambo:

**Umauti:** Ni mwisho wa kile alie hai hapa duniani, amesema Allah –Mtukufu-: "**Kila nafsi itaonja kifo**" [Aal Imran: 185], akasema tena: "**Kila alie juu ya ardhi ni mwenye kufa**" [Al-rahman: 26], na alisema kumuambia Nabii wake –Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-: "**Wewe ni mwenye kufa na wao pia ni wenye kufa (30) Kisha nyote siku ya kiyama kwa mola wenu mtashitakiana na**

**kuzozana (31)”** [Al-zumar], hakuna mwanadamu yeyote ataeishi milele duniani, amesema Allah – Mtukufu-: **“Hatukujaalia mwanadamu yeyote kabla yako kuishi milele”** [Al-anbiyai: 34], inapasa kuashiria mambo kadhaa, miongoni mwa hayo ni:

1) Hakika watu wengi wameghafilika na kifo, pamoja na kwamba kifo ni jamba la uhakika lisilo na shaka, na hakuna ataebeba chochote kwenda nacho kaburini bali atabaki na matendo yake tu, yakiwa matendo mema atakuwa ni mwenye kustarehe na kufaulu na yakiwa ni matendo mabaya atakuwa amefeli na kupata hasara.
2) Hakuna mwanadamu anaejua siku yake ya kifo ila Allah peke yake, hakuna ajuae atakufa lini wala atakufa wapi, kwasabu hilo ni katika elimu iliyojificha (**ghaib)** ambayo hakuna anaeifahamu isipokuwa Allah –Mtukufu- tu.
3) Wakati wa kifo ukifika haiwezekani kukizuia au kukichelewesha au kukikimbia, amesema Allah – Mtukufu-: “**Na kila watu wana muda wao (wa kuondoka ulimwenguni) utakapo wafikia muda wao huo hawatakawia (hata) saa moja**

**wala hawatatangulia (kabla haujafika)”** [Aaraaf: 34].

4) Muumini akijiwa na kifo, humjia Malakul-mauti (Malaika aliewakilishwa kutoa roho) akiwa katika sura nzuri harufu nzuri, watakuja pamoja nae Malaika wakiwa wanambashiria pepo, amesema Allah –Mtukufu-: **“Hakika wale waliosema mola wetu ni Allah kisha wakanyooka sawa watateremkiwa na malaika wawaambie msikhofu wala msihuzunike furahini kwa pepo ambayo mmeahidiwa**” [Fuswilat: 30], ama kafiri atajiwa na Malakul-mauti kwa sura ya kutisha, sura nyeusi yenye mandhari ya kutisha, na watakuja pamoja nae malaika wa adhabu wakimbashiria moto, amesema Allah –Mtukufu-:“**Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na malaika wamewanyoshea mikono yao (na kuwaambia) zitoweni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu pasipo**

**haki na kwa vile mlivyokuwa mkizifanyia kiburi aya zake (ungeona namna gani walivyokuwa wakipapatika)**” [An-am 93].

Kikija kifo ukweli huonekana, na mambo yote yatakuwa wazi kwa kila mwanadamu, amesema Allah –Mtukufu-: “**Hata yatapomfika mmoja wao na umauti husema: mola wangu nirudishe (ulimwenguni) (99) Ili nitende matendo mema badala ya yale niliyo yaacha (hujibiwa na malaika akaambiwa): Hapana! Hakika hili ni neno tu analolisema yeye (aliye mwovu anapofikiwa na mauti) na mbele yao kuna maisha ya baada ya kufa (ya taabu kwa waovu ya raha kwa wema) mpaka siku watakapofufuliwa (100)**” [Al-Muuminun], kikija kifo, kafiri ama anaemuasi Allah atatamani arudishwe duniani ili atende mema lakini majuto hayatomsaidia baada ya kupita muda, amesema Allah: “**Utawaona madhalimu wakiiona adhabu husema je iko njia ya kurudi (ulimwenguni?)**” [Shura: 44].

**Kaburi**: Ni kituo cha kwanza cha Akhera, atae okoka hapo yanayokuja mbele ni mepesi, na asie okoka hapo yanayokuja mbele ni mazito, imepokelewa kutoka kwa Anas –Allah amridhie- kutoka kwa Nabii wa Allah –Rehma na amani za Allah ziwe juu yake- amesema: “Hakika mja

akiwekwa kaburini mwake na ndugu zake wakaondoka, hakika yeye husikia sauti ya viatu vyao" akasema tena: "Watamjia malaika wawili na kukaa nane, kisha watamuambia: Ulikuwa ukimzungumzaje huyu mtu? Akasema: ama muumini atasema: Nashuhudia yakwamba yeye ni mja wa Allah na mtume wake, akasema tena: Ataambiwa: Angalia yaliyokuwa makazi yako motoni, hakika amekubadilishia Allah na kukupa makazi yako ya peponi, akasema Nabii wa Allah – Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-: Ataziona sehemu zote mbili, ama kafiri au mnafiki, atakuwa anasema: Wala sijui, nilikuwa nikisema kama walivyokuwa wakisema watu wengine, ataambiwa: Hautayajua wala hautayasoma, kisha atapigwa nyundo ya chuma kati ya masikio yake, atapiga ukulele mmoja, atasikia sauti hiyo kila kiumbe isipokuwa Majini na Watu".

Na kurejea roho katika mwili wa mwanadamu akiwa kaburini ni katika mambo ya akhera ambayo akili ya kibinadamu haiwezi kutambua uhalisia wake, anatueleza Allah –Mtukufu- kuwa mwanadamu hupata neema akiwa kaburini endapo atakuwa ni muumini na kustahiki hiyo neema, na ataadhibiwa kaburini akiwa ni mwenye kustahiki adhabu ikiwa Allah hajamsamehe, amesema Allah –

Mtukufu-: “**Moto unaletwa kwao asubuhi na jioni, mpaka wakati wa kuhesabiwa, na siku ambayo kiyama kitasimama kutasemwa, (watieni motoni jamaa wa firauni ikiwa ni malipo ya matendo yao mabaya)**” [Ghaafir: 46], na amesema Mjumbe wa Allah –Juu yake rehma na Amani-: “Taka hifadhi kwa Allah kutokana na adhabu ya kaburini”, akili iliyo salama haipingi jambo hilo, kwani mwanadamu huwa anaona vitu vinavyokaribiana na hilo kwenye maisha yake, Mfano: Mtu akiwa amelala anaweza kuhisi kwamba anaadhibiwa adhabu kali na akapiga kelele na kuomba msaada ilihali aliekuwa jirani yake alihisi hilo kabisa, pamoja kuwepo kwa utofauti mkubwa kati ya kifo na uhai.

Na adhabu huwa vinaadhibiwa roho na mwili kwa pamoja, amesema Mjumbe wa Allah –Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Hakika kaburi ni kituo cha kwanza katika vituo vya akhera, akiokoka mja hapo yanayokuja baadae ni mepesi, na asipo okoka hapo basi yanayokuja mbele ni mazito”, hivyo basi yatakikana kwa Muislamu akithirishe kutaka hifadhi kwa Allah kutokana na adhabu ya kaburi, hasa akiwa kwenye swala kabla ya kutoa salam ya kumaliza, na apupie kujiepusha na maasi ambayo ndio sababu ya adhabu ya kaburini na motoni, na imeitwa adhabu ya kaburi kwa sababu

watu wengi huwa wanazikwa makaburini, ama aliezama, na alieteketea kwa moto, na alieliwa na wanyama wakali, na mfano wao, hawa wanaadhibiwa wakiwa Barzakh (maisha kati ya kifo na kufufuliwa).

Na adhabu ya kaburi ziko za aina mbalimbali, iko ya kupigwa nyundo za chuma au nyenginezo, kama vile kaburi kujazwa giza, na kutandikiwa moto, na ufunguliwa mlango wa moto, na kufananishiwa matendo yake mabaya na umbile la mtu mwenye sura mbaya na harufu mbaya, atakaa nae hapo kaburini, ilihali adhabu ikiendelea kama atakuwa ni kafiri ama mnafiki, na kama atakuwa Muumini mwenye maasi basi ataadhibiwa kiasi cha madhambi yake na huenda ikaisha adhabu hiyo.

Ama muumini yeye ataneemeka akiwa kaburini, na kaburi litapanuliwa na kujazwa nuru na ufunguliwa mlango wa pepo na kumfikia harufu yake nzuri, na hutandikiwa tandiko la peponi, na hufananishiwa matendo yake mema na sura ya mtu mzuri anaemliwaza hapo kaburini.

## KUTOKEA KIYAMA NA ALAMA ZAKE:

1- Mwenyezi Mungu hakuumba huu ulimwengu kwa ajili ya kubaki milele, Isipokuwa itafika siku yamwisho, na siku hiyo ndio siku ambayo kitatokea kiyama ndani yake, na siku hiyo ni hakika wala hainashaka kufika kwake Amesema Allah mtukufu: "**Hakika kiyama nichenye kuja, hakina shaka kuja kwake**" [Alghaafir: 59] **N**a akasema Allah mtukufu: "**Na wakasema wale ambao wamekanusha kufufuliwa kuwa kiyama hakitatujia, sema ewe Mtume uwaambie, ninaapa kwa mola wangu kitawajia**" [Assabai: 3]

Na kujua kiyama ni lini ujio wake ni miongoni mwa mabo ya siyojulikana ambayo anayajua yeye tu Allah, Nawala hakuna hata mmoja miongoni mwa waja wake aliyemjuza hilo, Amesema Allah Mtukufu: "**Wanakuuliza watu, ewe Mtume, kuhusu kipindi cha kiyama kwanjia ya kukikanusha, Waambie, Hakika ya mambo ni kwamba ujuzi wa kipindi cha kiyama uko kwa Allah mtukufu, Na ni lipi linalokujuza wewe, ewe Mtume kwamba huenda kiyama kitakuwa karibu**" [Al aazaabu: 63].

**2-** Hakitasimama kiyama isipokuwa kwa watu waovu na wabaya tu, na hilo hakika ya Allah –alietakasika na mapungufu- kabla ya kusimama kiyama atatuma upepo mzuuri ukizitoa roho za waumini, pale ambapo Allah anataka kuwamaliza viumbe vyake kwa kuwafisha (kifo) na kufika mwisho wa Dunia, Allah anamuamuru Malaika kupuliza baragumu (nalo nipembe kubwa) na watakapolisikia sauti yake watu wote watakufa, Amesema Allah mtukufu: ”**Nakutapulizwa kwenye baragumu na hapo atakufa kila alie mbiguni na ardhini, ispokuwa anaemtaka Allah mtukufu asife”** [Alzzumar: 68]**,** Na hiyo inakuwa siku ya Ijumaa, kisha baada ya hapo wanakufa Malaika wote na wala hakuna atakaebaki ispokuwa ni Allah mtukufu mwenye kutukuka.

3- Mwili wa kila mwanadamu utakufa na kwisha kwa kuliwa na Ardhi isipokuwa mfupa wa asili yake (naoni mfupa ambao unakuwa chini ya uti wa mgongo), ama miili ya Manabii hii hailiwi na Ardhi, Allah mtukufu atateremsha maji kutoka mbinguni miili itaota kutoka ardhini. Pale anapotaka Allah kuwafufua watu atamfufua Israafiil Malaika mwenye kuwakilishwa kwa kupuliza Baragumu na atapuliza Baragumu hilo mara ya pili hapo

watafufuka viumbe wote na watu watatoka kwenye makaburi yao kama walivyoumbwa na Allah mara ya kwanza wakiwa hawana bila viatu, bila nguo, ilhali hawajafanyiwa twahara (kutahiriwa), Amesema Allah mtukufu: " **Na kutapulizwa baragumu (mpulizo wa pili, hapo zirudishwe roho zao kwenye miili yao) wakitahamaki wanatoka makaburini mwao wakielekea kwa mola wao kwaharaka"** [Yaasin: 51]**.** Na wakwanza ambae itapasuliwa Ardhi kwa ajili yake nae ni Nabii Muhammad –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- Kisha wa kupekewa watu katika Ardhi yakukusanywa nayo ni Ardhi pana iliyotandikwa (tambarare) na litasogezwa jua kuwa karibu na viumbe.

Na watu watabaki kwenye Ardhi hiyo muda mrefu wakisubiri ufafanuzi kati yao na kuhesabiwa, kisha Allah atatoa idhini ya kulipana kati yao, Na itawekwa Swiratwa (Nayo ni daraja jembamba kuliko unywele na linamakali Zaidi kuliko upanga litawekwa katikati ya moto wa Jahannam) hapo watapita watu kulingana na matendo yao, Miongoni mwao kuna watakaopita kama kupepesa jicho, na wengine kama upepo, Na wengine kama vile Farasi mwenye kasi, Na miongoni mwao wapo watakaopita

wakitambaa kwa magoti na mikono yao, Na kwenye Swiratwa kuna mahonga ambayo yanawavuta watu na kuwatupia kwenye moto wa Jahannam, Na watangukia kwenye moto huo makafiri na wale anao wataka Allah miongoni mwa waumini waliomuasi hapa duniani, Ama Makafiri watabaki kwenye moto milele, na ama waumini waliomuasi Allah wataadhibiwa kwenye moto kwa kiasi ambacho anakitaka Allah mtukufu kisha watatolewa na kuingizwa Poponi.

Na watasimama wale ambao wamevuka moto kupitia daraja hilo (nao ni watu wa peponi) juu ya kizuizi kilichopo kati ya pepo na moto kwanamna ambayo kila mmoja atamlipa mwenzie haki zake, na wala hatoingia peponi yule ambae amemdhulumu ndugu yake muislam mpaka amlipe haki yake, na kuridhia nafsi zao kwa wengine, Na watakapoingia peponi watu wapeponi na wakaingia motoni watu wa motoni, Yataletwa mauti kwa sura ya kondoo na kuchinjwa kati ya pepo na mato, na watu wa peponi na motoni wakiangalia, Kisha kutasemwa: Enyi watu wa peponi mtakaa humo milele na wala hakuna kufa, Na nyie watu wa motoni mtakaa humo milele na wala hakuna kufa. Na lau mja yeyote anaweza kufa kwa furaha basi wangekufa watu wa peponi

kwa furaha waliyoipata, Na lau mja yoyote anaweza kufa kwa huzuni basi wange kufa watu wa motoni.

## MOTO NA ADHABU ZAKE:

Amesema Allah mtukufu**: "Uwogopeni moto (**kwa kumuamini Mtume – Rehema na amani za Allah ziwe juu yake - Na kumtii Allah mtukufu**) Moto ambao kuni zake ni watu na mawe umeandaliwa kwa wenye kumkanusha Allah mtukufu na Mtume wake"** [Albaqarh: 24], Na amesema mjumbe wa Alla –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kuwaambia Maswaaba zake: "Moto wenu huu (ambao anauwasha mwanaadamu) ni sehemu moja tu miongoni mwa sehemu sabini za ukali wa moto wa Jahannam" wakasema: Tunaapa kwa Allah ingekuwa kwa ukali huu ungetosha Ewe mjumbe wa Allah, Akasema: Hakika moto huo umezidiwa ukali wake mara sitini na tisa na zote zina ukali kama huu"**.**

Na moto unatabaka saba, na kila tabaka ina adhabu kali kuliko nyengine, Na kila tabaka inawatu wake kutokana na kiasi cha matendo yao, Na wanafiki watakuwa daraja la chini kwenye moto, na ndio kwenye adhabu kali kuliko, Na Adhabu ya moto kwa makafiri ni yakudumu kila wakati haikatiki, Na

kila ambapo wanaungua wanarudishwa tena kwaajili ya kuongezewa Adhabu, Amesema Allah mtukufu: "**Kila zikiungua Ngozi zao tunawabadilishia Ngozi nyengine ili adhabu yao na uchungu vipate kuendelea"** [Annisaa" 56], Na amesema Mtukufu**: " Na wale waliomkanusha Allah mtukufu na mtume wake, watakuwa na moto wa Jahannam uliowashwa. Hakutatolewa uwamuzi kuwa wao wafe wakafa na kupumzika. Wala hawata punguziwa adhabu yake. Mfano wa malipo hayo, Allah mtukufu anamlipa kila mwenye kuendelea kwenye ukafiri"** [Faatwir: 36], na hufungwa wakiwa humo , na itafungwa mikono yao shingoni mwao, Amesema mtukufu: **"Na utawaona, ewe nabii, waasi siku ya Kiyama wamefungwa pingu mikono yao, miguu yao imekutanihswa Pamoja kwa minyororo na hali wakiwa wanyonge (49) Vazi lao nila rojo la mafuta linalochoma sana, na hapo moto utazichoma nyuso zao"** [Ibrahiim: 50]**,** Na chakula cha watu wa motoni ni matunda ya mti wa Zaqqum**,** Amesema Allah mtukufu**:**

**"Hakika mti wa Zaqqum (unatoka kwenye shina la moto wa Jahannam) (43) Matunda yake ni chakula cha mwenye madhambi mengi (44) Matunda ya mti wa zaquum ni kama madini**

**yaliyoyeyushwa, yanachoma ndani ya matumbo ya washirikina (45) Kama vile maji yaliyofikia upeo wa joto kwa kuchemshwa (46)** [Aldukhaan] Na inabainisha ugumu wa adhabu ya moto, Na ukubwa wa neema za Pepo, kwa yaliyokuja kutoka kwa Nabii- rehema na amani za Allah ziwe juu yake- kwamba yeye alisema: "Ataletwa aliekuwa na neema za duniani katika watu wa motoni siku ya kiyama kisha atazamishwe kwenye moto mara moja, Kisha aambiwe: Ewe mwanadamu, je umeona kheri yoyote? Je zilikupitia neema zozote? Atasema: hapana, Naapa na ewe mola. Na ataletwa aliekuwa na Maisha mabaya Zaidi hapa duniani katika watu wa Peponi na atazamishwa Peponi mara moja, Na ataambiwa ewe mwanadamu, Je umeshawahi kuona ubaya wowote? Je iliwahi kukupitia shida yeyote? Atasema: Hapana naapa ewe mola, Haijawahi kunipitia ubaya wowote? Walasijaona shida wewote" Kwa sababu hiyo Kafiri anapokuwa motoni anasahau neem na Maisha mazuri yote aliyopitia kwa kule kuzamishwa motoni mara moja tu, Na Muumini anasahau kila hali gumu aliyopitia Duniani kutokana na mabaya, ufakiri na kutokana na kuzamishwa Peponi mara moja tu.

## PEPO NA NEEMA ZAKE:

Pepo ni nyumba ya kudumu na heshima, Ameiandaa Allah kwa ajili ya watu wake wema, Ndani ya pepo hiyo kuna Neema ambazo hakuna jicho la mtu yeyote lililoona, wala sikio kusikia, na wala haijawahi kupita kwenye akili ya mja yeyote, Amesema Allah mtukufu: "**Hakuna nafsi yoyote inayoyajua yale aliyoyawekea Allah mtukufu hawa waumini ya kutuliza macho na kufurahisha moyo, yakiwa ni malipo yao kwa matendo yao mema"** [Alssajidah: 17]**,** Na hiyo Pepo ina madaraja ambayo wanatofautiana waumini kwa nafasi zao ndani yake kwa kiasi cha matendo yao, Amesema mtukufu: "**Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu na wale waliopewa ilimu watapata daraja zaidi**" [Al-mujaadila: 11]**,** Wanakula na kunywa ndani ya pepo vile ambavyo nafsi zao zinatamani, Ndani ya Pepo kuna mito kutokana na maji yasiyo haribika rangi na ladha yake, Na mito mingine itokanayo na maziwa haiharaibiki ladha yake, Na mito ya Asali iliyo safi, na mito inayotokana na pombe yenye ladha kwa wanywaji, Na pombe yao sio kama pombe iliopo Duniani, Allah mtukufu amesema**: "Zinazungushwa kwao glasi za Pombe inayotoka**

**kwenye mito inayotembea (45) Ni nyeupe rangi yake, ni tamu katika kuinywa (46) Haina madhara yeyote ya akili wala mwili, (47)** [Asswaaffaatu]**,** Na humo watawaoa wanawake wa Peponi**,** Amesema Mjumbe wa Allah**-** Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- **"**Lau mwanamke miongoni mwa watu wa Peponi atatokeza kwa watu walio Ardhini angeviangazia vilivyomo kati ya Mbingu na Ardhi, na angevijaza harufu nzuri**".**

Na Neema iliyo kubwa kwa watu wa Peponi ni kumuona Allah -alietakasika na kutukuka- na watu Peponi hawajisaidii haja ndogo wala kubwa na wala hawatoi kamasi na wala hawatemi mate, na vitana vyao vinatokana na dhahabu, na jasho lao ni miski, Na neema zao hizi ni zakudumu hazikatiki na wala hazipungui, Amesema mjumbe wa Allah – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- **: "**Ambae ataingia Peponi ataneemeka wala hakuna ubaya ndani yake, Hazichakai nguo zake wala haumaliziki ujana wake**",** Na atakaepata kiwango cha chini katika watu wa Peponi –Nae ni yule atakaetoka motoni mwisho miongoni mwa waumini na akaingia Peponi- ni bora Zaidi kuliko kupata mara kumi ya Dunia.

# MWANAMKE KWENYE UISLAMU:

Kabla ya kuzungumzia haki za Mwanamke kwenye Uislamu, Hakuna budi tubainishe baadhi ya mitazamo ya nyumati nyengine kwenye kumuelekea mwanamke, na walikuwa wakiamiliana nae vipi. Hakika Mwanamke alikuwa kwa Wayonani akiuzwa na kununuliwa, na wala hakuwa na haki yeyote, bali ilikuwa haki zote ni za Mwanamume, kama alivyokuwa akizuiliwa kupata haki yake kwenye miirathi, au haki ya kutumia mali.

Na hakika amesema mwanafalsafa wao maarufu anaeitwa **Saqraatwi:** “Hakika kuwepo kwa Mwanamke ndio sababu kuu na chanzo cha kuporomoka kwa maadili kwenye Ulimwengu, hakika mwanamke anafanana na mti wenye sumu kiasi kwamba unakuwa nje yake ni mzuri unapendeza, lakini endapo ndege wataula huo wanakufa muda huo huo”.

Ama Waroma walikuwa wanaitakidi kuwa mwanamke hana roho na wala mwanamke kwao hana nafasi yeyote na wala hana haki, na hakika ilikuwa alama zao: “**Mwanamke hana roho**” na kwa maana hiyo ndio walikuwa wakiwaadhibu wanawake kwa kuwamwagia mafuta ya moto

mwilini, na kuwafunga kwenye viguzo vya miti, pia walikuwa wakiwafunga wanawake wasiokuwa na hatia kwenye mikia ya Farasi na kuwaburuza mpaka wanakufa.

Na hivi ndivyo ilivyokuwa mtazamo wa Wahindi kwa Mwanamke, bali wao walizidisha Zaidi ya hayo walikuwa wakimchoma mwanamke pale tu anapofiwa na mumewe, Na hakika Wachina walimfananisha mwanamke Na maji yenye kuumiza ambayo yanaiosha (kuiondoa) furaha na mali, na Mchina alikuwa na haki ya kumuuza Mkewe, kama alivyokuwa na haki ya kumzika hali ya kuwa yuko hai.

Ama Mayahudi wao wanamuhisabu mwanamke kuwa ni mwenye kulaaniwa, kwasababu yeye alimhadaa Adam na kumfanya ale tunda kwenye mti aliokatazwa. Kama wanavyo muhisabu kuwa ni Najisi pale anapopata hedhi, anainajisi nyumba na kila anachokivaa, pia hawezi kumrithi baba yake kitu chochote, pale atakapokuwa na kaka zake.

Ama kwa Manaswara (wakristo) wanamuona mwanamke kuwa ni Shetani, na hakika amesema mmoja wa watu wa Dini ya Kinaswara: “Hakika mwanamke hana maingiliano na Jinsia ya

kibinadamu”. Na akasema Mtakatifu **Bonaventure**: (Mtakapo muona mwanamke wala msidhani kuwa mmemuona kiumbe wa kibinadamu, bali wala si mnyama, hakika huyo mnaemuona ni Shetani, na sauti mnayoisikia ni mlio wa nyoka) Na hakika waliendelea kuishi kwa mujibu wa kanuni ya Uingereza, mpaka katikati ya karne iliyopita, wakiwa hawahisabiki kuwa Raia. kama vile ambavyo hakuwa na haki za kibinadamu, wala hana haki za kumiliki kitu chochote hata mavazi yake ambayo anayavaa, Na hakika lilianzisha sheria Bunge la Skotland la mwaka 1567m, yakwamba: Haifai kwa mwanamke kupewa uongozi wowote ule, kama Bunge la Uengeza lilivyonyima mwanamke kusoma Injili, wakati wa utwala wa Henry wa nane, kwa sababu mwanamke ni Najisi. Na kwenye mwaka 586m Wafaransa waliweka kongamano kwa ajili ya kufanya uchunguzi: Je! Mwanamke ni mtu au sio mtu!? Na wakapata kuwa ni mtu lakini ameumbwa kwa ajili ya kumtumikia mwanamume. Na kanuni za Uingereza hadi mwaka 1805m zilikuwa zikihalalisha mwanamume kumuuza mkewe, na iliwekwa thamani maalum ya mwanamke kuwa ni Pensa sita (nusu shilingi).

Ama kwa upande wa Waarabu kabla ya Uislamu, hakika alikuwa mwanamke ni mwenye kudharaulika, harithi, na wala hatiliwi umuhimu na wala hana haki yoyote kwenye jamii, bali wengi wao walikuwa wakiwazika Watoto wao wakike wakiwa hai.

Kisha ukaja Uislamu ili kuondoa hizi dhulma zote juu ya mwanamke, Na kwa ajili ya kubainisha kwamba mwanamke na mwanaume ni sawa, yeye ana haki zake kama vile mwanamume alivyokuwa na haki zake, Amesema Allah mtukufu: "**Enyi watu, hakika sisi tumewaumba nyie kutokana na mume mmoja na mke mmoja, (Adam na Hawa) na tumewafanya nyinyi kwa kuzaana kuwa mataifa na makabila mbalimbali ili mjuane nyinyi kwa nyinyi, hakika mbora wenu kwa Allah mtukufu ni yule anaemcha yeye zaidi, hakika Allah mtukufu anawajua sana wacha Mungu na anawatambua)** [Alhujraat: 13]**,** Na Akasema Allah mtukufu**: "Na mwenye kufanya matendo mema, awe ni mwanamume au mwanamke hali ya kuwa anamuamini Allah mtukufu, basi hao Allah atawaingiza peponi na hawatapunguziwa chochote katika thawabu za matendo yao hatakama ni kiasi cha kitone kilichoko kwenye**

**kokwa ya tende”** [Alnnisaau: 124]**,** Na akasema alietakasika na mapungufu: **”Na tumemsihi binadamu awatendee wema wazazi wake wawili na awe mwema kwao kwa maneno na vitendo)** [Alankabuut: 8]**.**

Na akasema mjumbe wa Allah– Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake**-: “**Mkamilifu wa Imani kwa waumini ni yule aliekuwa mzuri wao kitabia, Na watu bora kwenu ni wale wabora wenu kwa wake zao kitabia**”** Na mtu mmoja akamuuliza Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-, Akasema: Ni nani mwenye haki ya kutendewa wema zaidi? Akasema: “Mama yako” Akasema kisha nani? Akasema: “Mama yako” Akasema kisha nani? Akasema: “Mama yako” Akasema kisha nani? Akasema: “Baba yako**”**.

Huu ndio mtazamo wa Uislam kwa ufupi juu ya mwanamke.

## HAKI ZA MWANAMKE KIUJUMLA:

Hakika mwanamke katika Uislamu ana haki zake kiujumla, miongoni mwa haki hizo ni:

1- Haki yake ya kumiliki: Mwanamke ana haki ya kumiliki chochote atakacho kama vile: Nyumba, Mashamba, Viwanda, Bustani, Dhahabu na Fedha na aina za Wanyama, sawa sawa ni mke wa mtu, au mma, au mtoto au ni dada.
2- Haki yake ya kuolewa, kuchagua mume, kujivua kwa mumewe, na kudai talaka ikiwa anapata madhara kwenye ndoa, Na hizi ni haki zilizothibiti kwa mwanamke.
3- Haki yake ya kutafuta elimu kwa kauli ya Mtume –Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake: “Kutafuta Elimu ni lazima kwa kila Muislamu”.
4- Haki yake ya kutoa sadaka kwenye mali yake kwa chochote atakacho, kujihudumia mwenyewe kwenye mali yake, Na kwa yeyote

yule amtakae kama vile: mume, Watoto, kina baba na kina mama.

5- Haki yake ya kuusia theluthi ya mali yake wakati wa uhai wake, na kutekelezwa usia huo baada ya kufa kwake bila kupingwa, kwa sababu usia ni haki ya mtu binasfi, na kama inavyokuwa kwa mwanamume ndio inakuwa kwa mwanamke, kwa sharti wasia usizidi theluthi ya mali (⅓ ya mali) mwanamke na mwanamume ni sawa.

6- Haki yake kwenye mavazi, Ni haki yake mwanamke kuvaa chochote anachokitaka katika hariri na dhahabu, ambavyo ni haramu kwa wanamume, kwa sharti mwanamke ajiebushe uvaaji utakaozingatiwa kuwa ni uchi kisheria, mbele ya yule ambae haruhusiwi kuvaa hivyo mbele yake.

7- Haki yake ya kujipamba na kuvaa mapambo mazuri Zaidi ya kifahari ayapendayo.

8- Haki yake ya kunywa na kula, mwanamke anakunywa chenye ladha na kizuri na atakula hivyo hivyo, hakuna tofauti kati yake na

mwanamume katika vyakula na vinywaji, kilicho halalishwa miongoni mwa viwili hivyo, na hivyo ni kwa ajili ya Mwanamume na Mwanamke, na kilicho haramishwa kwenye viwili hivyo basi ni haramu juu yao wote wanawake na wanaume.

Amesema mtukufu: “**Na kuleni na kunyweni (katika vizuri alivyowapa Allah mtukufu) na wala msikeuke mipaka wa wastani, kwani Allah mtukufu hawapendi wakeukaji wenye kupitisha kiasi katika vyakula na vinywaji na vyenginevyo”** [Al aaraafu: 31]**,** Na mazungumzo haya yanakusanya jinsia zote mbili (mke na mume).

9- Haki yake ya kurithi na kurithiwa.

## HAKI ZA MKE KWA MUMEWE:

Hakika haki maalumu za mke ni zile haki zake kwa mumewe, Hizi ni haki ambazo analazimika kuzitekeleza kwa mumewe ikiwa kama vile malipo ya haki alizo tekelezewa na mumewe.

Na hizi ni baadhi ya haki zilizo muwajibikia mwanamke kwa mumewake kwa kauliya Allah

mtukufu: "**Na wanawake wanahaki kwa waume zao kama waume walivyo na haki kwa wake zao kwanjia ya wema**" [Albaqarah: 228], Inapaswa kwa Mume kuzipokea na kuzitekeleza kwa mke wake kiukamilifu, isipokuwa mke ataposamehe baadhi ya haki anaweza kufanya hivyo:

1- Kumuhudumia mke kulingana na hali ya wepesi na uzito wa maisha, Na yanaingia kwenye huduma mambo yafuatayo: Mavazi, Chakula, Kinywaji, Dawa na Makazi.
2- Kulinda heshima ya mke wake, mwili wake, mali yake, na Dini yake.
3- Kumfundisha yaliyo lazima kuyajua katika mambo ya Dini, Na endapo atashindwa kulifanya hilo yeye mwenyewe, Atampa idhni ya kujifunza kwa kuhudhuria vikao vya elimu vya wanawake kwenye nyumba za Allah (misikiti), au Madrasa au vyenginevyo.
4- Kuishi nae vizuri, kwa mujibu wa kauli ya Allah mtukufu: "**Na ishini nao kwa wema**" [Annisaau: 19]**,** Na miongoni mwa kuishi kwa wema ni kuto zivunja haki zake, ikiwemo tendo

la ndoa, na kuto muudhi kwa matusi, kumpuhuza na kumdharau. Na miongoni mwa kuishi nae vizuri ni kutomzuia kuwatembelea jamaa zake wa karibu endapo haogopei fitna kwa mkewe, na wala asimlazimishe kufanya kazi asizoziweza, na amfanyie vizuri kwenye maneno na matendo, kwa mujibu wa kauli ya Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Mbora wenu ni yule alie mbora kwenu kwa familia yake, na mimi ni mbora wenu kwa familia yangu”.

## HIJABU:

Hakika Uislamu ulipupia Zaidi kutengeneza familia kutokana na mipasuko na miporomoka ya kimaadili, ukaiwekea uzio madhubuti, ambao ni adabu na tabia njema, ili nafsi zibaki kuwa salama, na Jamii iwe safi, haiongozwi na matamanio wana tabia za kimaumbile, hakika Uislamu umeweka vizuizi kwa ajili ya kuzuia visababishi ambavyo vinapelekea kwenye fitna (uovu), ukaamrisha kufumba macho kwa upande wa wanamume na wanamke.

Kama Allah alivyofanya hijabu kuwa ni sheria kwa mwanamke kwa ajili ya kumtukuza, na kumtengeneza kutokana na kudharaulika, na kumueka mbali na kuyapata wanayo yafanya mafisadi na watu walio na nafsi dhaifu, na kumuhifadhi juu ya wale ambao hawajui nafasi za ubora wala uzito mwanamke, na kufunga mlango wa Fitna ambao sababu yake ni kujipamba wa, na kudhihirisha yanayo fitinisha, na kwa kumuekea uzio unaolinda heshima na nafasi yake.

Hakika ya Uislamu ndio ambao unalazimisha Hijabu unataka kumuaminisha mwanamke Maisha mazuri, kwamba hakika mwanamke anapokua anapungua uzuri wake, na pale Mwanamume anapotoka njiani na akawaona wasichana wazuri kutokana na mapambo yao, wakati anapofika nymbani kwa mke wake anaanza kulinganisha alie muona na mkewe, na hili linafanya Nyumba nyingi kuharibika.

## NDOA YA WAKE WENGI:

Hakika lilikuwepo jambo la kuoa wake wengi tangu kuwepo kwa mwanadamu, na lilikuwepo pia kwenye sheria zilizotangulia kabla ya Uislamu, na hata kwenye jamii za zamani, kama ilivyokuwepo kwa

Mayahudi, Waktisto, Wachina, Wahindi na wengineo.

Na kulikuwa kuoa wake wengi hakuna idadi maalum, kiasi ambacho mume anaoa wanawake kwa idadi anayoitaka, kama ilivyo, Mwanamke alikuwa akidhulumiwa, Ndio ukaja Uislamu ukaondoa dhulma kwa mwanamke, na ukaweka idadi ya kuoa wake wengi isizidi wake wanne.

Na Uislamu ulipo halalisha kuoa wake wengi iliweka sharti, nalo ni uadilifu kati ya wanawake, na ukatoa tahadhari kubwa juu ya kuivunja sharti hiyo, ikaiwekea adhabu kali kwa asieitekeleza.

Kisha kuna dharura nyingi ambazo zinaweza kupelekea Mume kuongeza mke, kwamfano mke wa kwanza akiwa Tasa (hazai), au nimgonjwa au mfano wa hayo, Je lililokuwa jema kwa mke mwenye matatizo kama hayo ni mume wake kumuacha au ni kuoa mke mwengine?

Kama kulivyo kuoa wake wengi inaweza kuwa na maslahi kwa umma, kama vile kuzidi wanawake kutokana na vita au mengineyo, Na hakika vita vya Dunia kwamfano vimeacha wanawake (wajane) milioni (25) kwenye Nchi za Ulaya, Je lililobora ni

kubaki wanawake hawa bila kuolewa au ni kuolewa akawa mke wa pili? Bali kulifanyika maandamano ya wanawake kwenye nchi ya Ujerumani baada ya vita ya pili ya Dunia mnamo mwaka 1945m ambayo wanawake walitaka iuwekwe sheria (kikatiba) ambayo inahalalisha mwamume kuoa wake wengi kwa lengo la kumlinda mwanamke wa Kijerumani kutokana na kujulikana kwa uzinifu.

## KITU GANI UISLAM UNATAKA KWETU?

Uislam haumtaki Muislam aiache dunia kabisa, wala haumtaki akae Misikitini tu ili afanye Ibada, au akae kambi ya kivita tu ili kuutetea Uislam, sivyo hivyo! Bali Uislam unataka Waislam wawe wenye maendeleo bora,wawe mabwana walioendelea, na kiuchumi wawe matajiri zaidi, na kielimu wawe wasomi zaidi, na kila Muislam ajue haki ya mwili wake kwake, kuupa chakula na mazoezi, lakini pia haki ya kuiliwaza nafsi yake kwa aina mbali mbali za starehe za halali, na haki ya mke wake ya kumtunza na kuishi nae kwa wema, na haki ya mtoto wake ya kumlea na kumuelekeza na kuwa mpole kwake, na haki ya jamii kwa kufanya kila lenye

maslahi katika jamii, kama vile anavyotambua haki ya Allah ya kumpwekesha na kumtii.

Uislam unatufunza kuwa Allah ndie mmiliki wa huu ulimwengu, yupo huru kwa kufanya alitakalo katika ulimwengu wake, anahuisha na kufisha, je kuna yoyote ambae anaweza kujilinda na kifo, akapata kuishi milele? humpa maradhi mtu na humponya, Je! kuna yoyote anaeweza kumpa ponyo yoyote Yule aliezuiliwa ponyo na Allah? Na Allah hutoa mali na kuwajaribu watu kwa kuwafanya mafakiri, anapeleka mafuriko na pia kufanya maeneo mengine yawe kame, kila mwaka utasikia mafuriko yametokea kwenye baadhi ya maeneo, na mengine yamepata hali ya ukame.

Nani aliwazidishia maji hawa mpaka wakalalamika, na wengine akawazuilia kupata maji mpaka wakayatamani? nani alimpa Yule mtoto wa kike, na kumpa mwingine mtoto wa kiume, na mwingine kuwa tasa? Je! anaweza alieruzukiwa watoto wa kike kuwageuza kuwa wa kiume, na alie tasa anaweza kuzaa?

Allah pekee ndie anae waandikia kifo watu hali ya kuwa wao bado watoto wadogo, na huwapa maisha marefu wengine mpaka wanakuwa vikongwe, na

kutuma wimbi la baridi kali na barafu kwenye mji Fulani, na mji mwingine akatuma wimbi la joto kali, akaupatisha mji Fulani na tetemeko la Ardhi. Mambo yenye kuonekana wazi, Binadamu hana uwezo wa kuyaondoa au kuyazuia, kwa hiyo wanakiri watu wengi kwamba Allah ndie mmiliki wa ufalme, na ndie mwenye kuuendesha ulimwengu, lakini je huko kukiri tu kunatosha kupata mtu sifa ya kuwa yeye Muislam?

Hapana, bali lazima pia kukiri kuwa huyo Allah ndie anaepaswa kuabudiwa, ukikiri kuwa Allah yupo, na yeye ndie mola na mlezi wa viumbe wote, na kwamba yeye ndie mmiliki wa ufalme, basi usiabudu kingine asiekuwa yeye, wala usielekeze kwa asiekuwa yeye aina yoyote ya Ibada, Huu ndio Uislam.

Kwa hiyo kuamini ya kwamba Allah ndie mola mlezi wa viumbe wote, na yeye ndie mmiliki wa ulimwengu, ni katika matendo ya moyoni, itikadi anayoiamini mwanadamu, ama kuamini kwamba yeye ndie Mungu, haiishii kwenye kuamini tu bali lazima ivuke na kufika katika matendo na tabia za mtu, na kufanya ibada, na kumpwekesha Allah kwa kumuabudu, na mtu akiacha kumuabudu yeye na akakiabudu kisichokuwa yeye hatokuwa Muislam,

hata kama atakiri na kuamini kwamba Allah ndie mola mlezi wa viumbe wote na ndie mmiliki wa ulimwengu.

Na moyo ambao unakiri kuwa manufaa na madhara yote hayo hupangwa na Allah, kuhalalisha na kuharamisha ni miliki ya Allah, mapenzi kamili na hofu kamili na utii mkamilifu ni kwake tu Allah, moyo uliojaa kumtukuza Allah na unahisi nini maana ya neno (Mungu Mkubwa) basi kila kitu hukiona ni kidogo mbele ya Allah.

Na kwa vile kuna katika matendo ya mwanadamu yenye kuonesha kutukuza kulikokamilika, kama vile kuomba na kuswali, kurukuu na kusujudu, kuweka nadhiri na kuchinja, kumtakasa Allah na kumuepusha na kila ushirikina, hakika Muislam hayafanyi hayo isipokuwa kwa ajili ya Allah, basi haswali kwa ajili ya mtu yoyote, wala hasujudu na kurukuu isipokuwa kwa ajili yake, wala hamwambii mtu yoyote asiekuwa Allah: (umekamilika) wala hataki msamaha kwa madhambi aliyoyafanya isipokuwa kwake pekee, kwa sababu haya yote ni katika ishara za kutukuza kikamilifu, jambo ambalo ndio siri ya Ibada.

## UISLAMU UNAYABOMOA (KUYAFUTA) YALIYOKUWA KABLA YAKE.

Na katika fadhila za Allah na Rehema zake ni pale alipoufanya Uislam unayabomoa yote yaliyo kabla yake, miongoni mwa madhambi na maasi mbali mbali, kwa hivyo kafiri akisilimu tu basi Allah humsamehe kila kosa alilotenda zama za ukafiri wake, na kuwa msafi hana dhambi yoyote.

Na mtu aliyeneemeshwa na Allah kwa kuwa Muislam baada ya kuwa alichuma mali ya Haram, hakika hii mali inakuwa halali kwake, na wala hana dhambi yoyote kwa mali hiyo. si kwa kubaki nayo hiyo mali, wala kwenye ile aliyoitoa sadaka, wala kwenye ile aliyoolea, kwa sababu Allah mtukufu anasema: **“waambie wale walikufuru kama wataacha watasamehewa yale madhambi yaliyopita”** [Al anfaal: 38]. Maana yake kila yaliyotangulia katika madhambi watasamehewa.

Lakini ile mali ambayo aliipora kutoka kwa mtu maalum yampasa amrejeshee, ama ile mali ambayo aliichuma wakati akiwa kafiri kwa ridhaa za watu wenyewe, hata kama ikiwa ni ya haram, mfano mali ya riba au mihadarati au jambo lingine ambalo ni

haram kisheria basi hiyo inakuwa halali kwake - akisilimu- ataendelea kuimiliki.

Na mlango wa kutubu katika Uislam uko wazi hata kama huyu mja Muislam madhambi yake ni mengi mno, na mahitaji ya binadamu ya kutubu ni endelevu, kwa vile kila binadamu hufanya makosa, na mtu mwema katika wanaofanya makosa ni Yule anaetubia baada ya kufanya kosa. kama alivyosema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake-. Na kwa vile binadamu hana kinga inayomzuia kufanya madhambi, hakika Allah amemfungulia mlango wa kutubu, na amemwamrisha kufanya hivyo anapofanya kosa, Anasema Allah mtukufu: "**Sema enyi waja wangu waliojidhulumu nafsi zao msikate tamaa na rehema ya Allah, hakika Allah husamehe dhambi zote, hakika yeye ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu.**) [Al Zumar: 53]

## VIPI TUNAINGIA KATIKA UISLAM?

Na baada ya kujua utukufu wa dini ya kiislam, na kwamba hiyo ndio njia pekee ya kuokoka mbele ya Allah- mtukufu- na kwamba kuingia katika Uislam ni jambo la lazima kwa kila mtu, na kwamba hakuna njia ya kuingia peponi na kuokoka na moto siku ya kiama isipokuwa kwa kuingia katika Uislam, na jawabu la hilo ni kwamba ukitaka kuingia katika uislam ni juu yako tu kufanya haya:

Kuamini kwamba **hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa allah, na kwamba muhammad ni mjumbe wa allah**, na utamke hayo kwa ulimi wako, kisha uanze kujifunza sheria za kiislam na kuzitekeleza, mfano: kuswali nk. Na vitabu vya kujifunza hayo vipo vingi katika maktaba mbali mbali na vituo vya kiislam.

# VYANZO:

1. Dini ya uislam
2. Njia kuelekea kwenye uislam
3. Selabasi ya kielimu ya familia na jamii
4. Kuutambulisha uislam
5. Mkutano wa wazi, wa mwenye fadhila Sheikh Muhammad Bin Swalehe Al Uthaimini.

# FIHRISI YA KITABU:

UTANGULIZI .......................................................... 3
KWA NINI TUMEUMBWA?.................................... 5
NI NINI UISLAM?................................................... 6
KISA CHA KUUMBA.............................................. 6
MTUME MUHAMMAD- REHEMA NA AMANI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE: .................................... 10
UFUPISHO JUU YA NASABA YAKE NA MAISHA YAKE -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-: .... 11
MIONGONI MWA TABIA ZA MTUME MUHAMMAD -REHEMA NA AMANIA ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE-. ........................................................ 21
MIONGONI MWA MIUJIZA YA MTUME -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-: ................................ 25
MISINGI YA DINI YA KIISLAM .......................... 28
NGUZO ZA UISLAMU ........................................... 36
Maana ya nguzo za Uislamu.................................... 37
MIONGONI MWA SIFA (MAALUM) ZA DINI YA UISLAMU ...................................................... 40
MIONGONI MWA MAZURI YA UISLAMU ........... 49
a-Maamrisho ya Uislamu........................................ 50
Na yasiyokuwa hayo katika maamrisho mazuri ya Allah. ........................................................................ 52
b-Makatazo katika Uislamu.................................... 52
SIKU YA MWISHO ............................................... 55

KUTOKEA KIYAMA NA ALAMA ZAKE: ............. 62
MOTO NA ADHABU ZAKE: .................................. 66
PEPO NA NEEMA ZAKE:....................................... 69
MWANAMKE KWENYE UISLAMU:...................... 71
HAKI ZA MWANAMKE KIUJUMLA:.................... 76
HAKI ZA MKE KWA MUMEWE: .......................... 78
HIJABU: ........................................................... 80
NDOA YA WAKE WENGI:..................................... 81
KITU GANI UISLAM UNATAKA KWETU?........... 83
UISLAMU UNAYABOMOA (KUYAFUTA) YALIYOKUWA KABLA YAKE............................. 87
VIPI TUNAINGIA KATIKA UISLAM?................... 89
VYANZO: .......................................................... 90
FIHRISI YA KITABU: ........................................... 91